

KUNENA

KWA

LUGHA

HARRY W. LOWE

KUNENA KWA

LUGHA

*Historia Fupi ya Kioja Kijulikanacho
Kwa jina la
Glossolalia, au Kunena Kwa Lugha*

Harry W. Lowe

Mfasiri: M. Mwamalumbili

Speaking in Tongues - Kiswahili

YALIYOMO

- Sura ya 1 Hali Iliyopo Sasa.....
- Sura ya 2 Roho Mtakatifu Siku ya Pentekoste.....
- Sura ya 3 Ushahidi Mwingineo wa Agano Jipyा.....
- Sura ya 4 Karama ya Lugha Pale Korintho.....
- Sura ya 5 Agano Jipyा Hadi Matengenezo ya Kanisa.....
- Sura ya 6 Baada ya Siku za Matengenezo ya Kanisa.....
- Sura ya 7 Je, Hivi Itakuwako Pentekoste Nyingine?.....

SURA YA 1

Hali Iliyopo Sasa

“Sisi tuko mbali sana toka Pentekoste!

Hivyo ndivyo alivyosema mnenaji mmoja mwenye nguvu katika mkutano mkuu wa wachungaji wa madhehebu zote. Alikuwa akiisikitikia hali mbaya ya kiroho ambayo Ulimwengu wa Kikristo umeifikia, kushindwa kwake kuyakabili barabara matatizo ya kidunia, ubaridi wake kuelekea kwenye kazi kubwa mno ya kuupelekea injili ulimwengu mzima, kumezwa kwake katika anasa na kuipenda dunia. Mambo ya hakika aliyosema, pamoja na takwimu zake alizotoa zilikuwa zinavutia sana, na wasikilizaji wake walikuwa pamoja naye. Wakachukua maneno yake haya, “Sisi tuko mbali sana toka Pentekoste,” na mnenaji baada ya mnenaji akayarudia tena na tena.

Ni dhahiri kwamba Ukristo unaingia katika kipindi cha mgogoro mkubwa. Tungeweza kukijaza kitabu hiki kidogo na matatizo yaliyokubaliwa kwamba yapo - umaskini, ujinga wa kutokujua kusoma na kuandika, uhalifu, vita, udanganyifu, uasherati, chuki kati ya mataifa, migawanyiko ya kidini na kuchukia au kupenda bila kuwa na sababu ya busara: Juu ya matatizo yote hayo ni ile hofu inayotula kama kutu isemayo kwamba sisi tunaishi katika “ulimwengu ulioachwa na Mungu,” kama mnenaji mmoja alivyosema.

Ni hofu hiyo isemayo kwamba sisi tuko mbali sana na Mungu ambayo inachangia kuleta tatizo letu kubwa kuliko yote, kwa kadiri somo letu la sasa linavyohusika. Ubaridi huo wa kiroho unapovuka mahali fulani na kugeuka kuwa karibu ugonjwa wa kupooza kabisa ndani ya kanisa, basi, hapo ndipo mambo ya kila namna, mema na mabaya, yanaweza kutokea.

Kwanza, wale wachache amba ni wacha Mungu kweli kweli - na tuisahau ya kwamba daima Mungu anao waaminifu wake wachache - humlilia Mungu, wakisema:

“Njoo, Roho Mtakatifu, Ee Hua wa mbinguni
Pamoja na uweza wako uhuishao;
Washa mwali wa moto wa upendo mtakatifu
Ndani ya miyo yetu hii yenye ubaridi.”

Wacha Mungu wachache kama hao waliosalia wanaendelea na njia yao ya kutoa ushuhuda wao kwa maombi, hawauchi moto wa kiroho moyoni mwao kuzimika kutokana na hiyo gharika ya kuipenda dunia hii.

Pili, Wakristo wengi wa jina tu hupoteza mng’ao wao wa kiroho. Ama wanabaki katika hali ya kuganda kama barafu katika dhehebu lao, ama wanatanga mbali na Mungu na mbali na kanisa.

Kundi la tatu linatenda kwa njia nyingine. Wakiwa na wasiiasi huo mwangi wanaamua kufanya kitu fulani kuhusiana na hali hiyo. Uamuzi huo wa kufanya kitu fulani unastahili sifa, halafu unyofu wa moyo wa watu hao hautiliwi mashaka. Hawana furaha katika dhehebu lililo na “mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake,” nao wana “jiepush[al]” na watu kama hao ili kutafuta njia mpya ya kuingia mbele za Mungu. 2 Timotheo 3:5. Ni jambo la hakika kwamba kuna joto kidogo sana, pamoja na uwezo wa kiroho ndani yetu sisi tunaojiona kuwa bora kabisa, nasi tunayo haja ya kumtafuta Mungu kwa bidii zaidi. Yatupasa kuondokana na utupu huo, kutojali, na dhambi, mambo ambayo yanawasumbua Wakristo wengi mno siku hizi. Tutafanya nini basi? Tutapata wapi dawa ya kututibuu?

Shaiku ya Kupata Uamsho na Matokeo Yake

Uzoefu wa Siku ile ya Pentekoste katika Matendo 2 umetia msukumo wa kila namna wa kuwapo kwa matapo [makundi] ya uamsho, ya zamani pamoja na yale ya sasa. Watu wanataka kupata uwezo ule alioutoa Mungu alipolianzisha kanisa la Kikristo katika dunia hii, nao wanachukua njia mbalimbali ili kuupata. Baadhi ya matokeo yamekuwa ya kushangaza sana.

Juhudi za siku hizi za kutaka kupokea “*ubatizo wa Roho*” ule wa Agano Jipyä mara nyingi zinakuwa katika mfumo wa “*karama ya lugha*.” Katika jumuia nyingi zaidi za Kikristo za siku hizi, kama vile mionganini mwa Waanglikana, Wapresibiteri, na Walutheri, *kunena kwa lugha* huitwa “*glossolalia*,” neno linalotokana na maneno mawili ya Kigiriki, *glossa* likimaanisha “*lugha*,” na *laleo* likimaanisha “*kunena*.” Katika jumuia zizo hizo jambo hilo pia huitwa “*Uweza wa Mungu Unaofanya Upya*” (the Charismatic Renewal) kutokana na “charisma” [karisma], yaani, kipawa cha neema yake Mungu.

Baadhi ya matokeo ya ajabu ya kuonekana kwa karama hiyo ya lugha yaliandikwa katika gazeti la *The Saturday Evening Post*, la Mei 16, 1964. Watu waliokuwa wakitafuta uwezo wa Mungu kwa njia hiyo walikuwamo na wachungaji toka katika madhehebu zile kubwa, walikuwapo na wanafunzi wa Chuo Kikuu, vizito, na wengineo.

“Jambo mojawapo ambalo si la kawaida kabisa kuhusu uamsho huo unaoendelea sasa, kwa hali yo yote ile,” linasema gazeti hilo la *Post*, “ni namna huko *kunena kwa lugha* (glossolalia) kulivyoruka mipaka na kwenda nje ya mwelekeo wake ule wa Pentekoste. Kukiyaruka makanisa yale ya daraja la kati, kumejitokeza kwa namna ya kushangaza sana katika kundi lile la jamii ya vizito lililo katika jumuia za Kikristo - Kanisa kubwa la Anglikana linaloheshimika sana, ambalo washiriki wake kwa sehemu kubwa wanatoka katika mazingira bora kabisa kiuchumi, kijamii, na kielimu.”

Madhehebu kama arobaini hivi yaliyotengana yanasmekana kwamba yameathirika. *Misisimko ya ajabu kihisia na kimwili* imeripotiwa kutoka katika vyanzo vingi. Mchungaji mwenye umri wa miaka arobaini na nane wa Kanisa la Kibaptisti la Imanueli katika Nyanda za juu za Atlantiki, kule New Jersey, mtu mwenye afya mbaya, alisimulia kwamba “kitu fulani mfano wa umeme kilishuka chini katika uti wangu wa mgongo” wakati mchungaji mwenzake alipoweka mkono wake juu ya kichwa cha mtu huyo wa kwanza na kumwomba Roho aje. Asubuhi iliyofuata aliamka akiwa anatokwa na jasho mwili mzima, na wakati alipokuwa akitoka kuoga, anasema, “Niliona maono ya mashine moja ichapishayo yenewe habari katika utepe, nami niliona maneno haya ‘Sa-da-ma-li’ yamechapishwa. Nilipoyatamka maneno hayo, matamshi machache mengine zaidi yakaja yenewe kinywani mwangu.” Mara tu baada ya tukio hilo, Dk. Howard M. Ervin aliyatumia maneno haya katika sala yake: ‘*Shan dama lai kushaiah hodhaiah salamah maqaiah shan dama lai maqaiah muriah.*’

Jambo hilo, moja mionganini mwa mifano mingi, lilikuwa kielelezo cha jinsi maneno “*yasiyokuwa sehemu ya lugha yo yote ya kibinadamu inayojulikana*, yanavyosadikiwa na maelfu ya watu kuwa huo ni utimilizo wa siku hizi wa maneno haya katika Matendo 2:4: “Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, *wakaanza kusema kwa lugha nyiningine, kama Roho alivyowajalia kutamka.*”

Katika mwezi ule wa Januari, 1964 katika mji wa Landani, Uingereza uliitishwa mkutano wa kawaida wa Baraza la Wachungaji wa Ailing’toni (Islington), na hotuba iliyosifiwa sana juu ya Roho Mtakatifu ilitolewa na Mchungaji Yohana Stoti (John Stott). Hotuba hiyo imekuzwa na kupatikana kama kijitabu chini ya kichwa hiki *The Baptism and Fullness of the Holy Spirit* (Ubatizo na Utimilifu wa Roho Mtakatifu), kimechapishwa na Inter-Varsity Fellowship (bei ilikuwa shilingi mbili – 1964). Mwandishi anakanusha dai lisemalo kwamba “*ishara muhimu kabisa ya kuonyesha kuwa mtu amempokea Roho ni ‘kunena kwa lugha.’*” Dai hilo linawafanya watu kuhitimisha kwa kusema kwamba Wakristo wale wasioitumia karama hiyo ya lugha, hawajampokea Roho katika utimilifu wake

wote. Bwana Stoti anasisitiza kwa nguvu kwamba kuwako kwa Roho Mtakatifu katika maisha ya mtu ni kwa lazima sana, tena ni kwa kudumu kuliko kule “kunena kwa lugha,” kwa sababu kunabadilisha maadili ya maisha yote ya mtu kuliko kuonekana tu katika kioja fulani cha muda kinachopita upesi.

Wenye Mamlaka Watoa Maonyo

Matukio hayo ya *kurukwa na akili* yameenea mahali pengi mno, tena yamejaa *misisimko mingi mno* hata ikamlazimu Askofu James A. Pike wa Kanisa la Anglicana kule Kalifonia (California) atoe mwongozo ambao unapiga marufuku kabisa kuomba kwa lugha. Alitangaza kwamba desturi ile iligeuka na kuwa ya “hatari kwa amani na umoja wa kanisa” na “tishio kwa mafundisho sahihi na sera zake.”

Dk. William Culbertson wa Chicago, Rais [Mwenyekiti] wa Taasisi ya Biblia ya Moody inayozishikilia kanuni zake, aliwaonya wanafunzi wote dhidi ya kuomba kwa lugha. Viongozi wengine wametoa maonyo kama hayo.

Watetezi wa desturi hiyo wanaonyesha kwamba upinzani toka kwa wenye mamlaka wa kanisa unaweza kutarajiwa kwa sababu viongozi wale wa Kanisa wa Kiyahudi walipinga matokeo yale ya Pentekoste yaliyolelezwa katika Matendo 2, kwa kutoa kashfa, wakisema: “Wamelewa!” Matendo 2:13.

Wenye mamlaka wengine wanasita kulaani matokeo yanayotokana na shakuu ya watu itokayo moyoni ya kupata uzoefu wenye kina zaidi wa kiroho. Wanayaangalia matokeo kwa moyo ulio na mawazo huru. Ni dhahiri kwamba wachungaji wengi mashuhuri pamoja na walei [washiriki wa kawaida] ambao mpaka sasa hawafikiriwi kuwa wako katika “jamii ya Kipentekoste,” wamekiunga mkono waziwazi kioja hicho kipyta. Ingawa hawaajungana katika mafundisho yao ya dini, wanaonekana kuukubali msemo usemao kwamba *utakaso wa kweli unafikia kilele chake katika uzoefu unaomfanya mtu kurukwa na akili ambao mwisho wake ni katika karama hiyo ya lugha*. Kwao Roho Mtakatifu hapatikani katika “kutulia na kutumaini” (Isaya 30:15), bali katika maonyesho ya nje ya kurukwa na akili kwa kupagawa, na wakati mwingine kwa kuumbua uso au kujinyonganyonga, na kwa kutumia lugha zinazojulikana au zisizojulikana. Ni msisimko huo usio na utaratibu ambao huonekana kuwa haufai kwa viongozi wenye makanisa yanayotumia liturjia [utaratibu wa dini wa ibada na sala kabla ya mahubiri kutolewa]. Maoni yao juu ya ibada yanaelezwu kwa maneno haya ya mtume Paulo: “Mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu.” 1 Wakorintho 14:40. Kwa nasibu, shauri hilo la mtume lilitolewa kwa kanisa lile la Korintho kuhusiana na namna walivyoitumia karama hiyo ya lugha.

Dokezo jingine kuhusu wasiwasi walio nao viongozi wa kanisa ambao unazidi kuongezeka unaonekana katika hatua iliyochukuliwa na Sinodi ya Kilutheri. Ilitangazwa mjini New York mapema mwaka 1964 kwamba kwa sababu Walutheri wengi mno wanajizoeza katika msukumo huo wa kunena kwa lugha, basi, ruhusa imetolewa kufanya utafiti huo, na kwamba bodi ilikuwa imeteuliwa kufanya uchunguzi kamili, usiopendelea upande wo wote juu ya maonyesho hayo. Bodi hiyo ilitakiwa kuchunguza, mionganii mwa hoja nyingine, aina ya watu wanaohusika katika uzoefu huo halisi. Ingejaribu kuthibitisha iwapo aina ya watu wenye hisia zinazofanana za maisha yao ya nyuma ndio walioathirika kwa sehemu kubwa. Fedha taslimu zinazofikia maelfu mengi ya dola hazitumiki kwa njia hiyo isipokuwa kama kanisa hilo limetikiswa vibaya sana kiasi cha kufanya uchunguzi wa kitu fulani ambacho hakiwezi kuelezwu kirahisi.

Kuna maswali ambayo, Wakristo wenye akili katika siku hizi za hatari kubwa, ni lazima kutafuta jibu. Je, ni kwa kusudi gani Roho alimwagwa juu ya Kanisa Siku ile ya Pentekoste? Je, Roho Mtakatifu alikuwa ni kipawa cha kudumu ndani ya kanisa? Je, karama ya lugha ilikusudiwa kuwa

ishara muhimu na ya kudumu inayoonyesha kuwako kwake Mungu katika kanisa lake? Je, kipawa hicho cha Pentekoste kilikuwa ni ishara kwa Wayahudi, kwa Mataifa, au kwa wote wawili? Je, karama ile ya lugha ilionekana baada ya Pentekoste, na kama jibu ni ndiyo, je, ni kwa muda gani? Je, lugha zile zilizonenwa wakati ule wa Pentekoste zilikuwa zinajulikana au hazijulikani na watu? Je, historia ya kanisa inatufunulia nini kuhusu karama hiyo ya lugha katika vizazi vyote? Je, ni habari gani tuliyo nayo kuhusu maonyesho (ishara) haya tunayoyaona siku hizi ya karama hiyo ya lugha?

Tutajitahidi sana kuyajibu maswali hayo katika nuru ya maelezo kama yale tuliyo nayo katika Agano Jipyä na katika kumbukumbu za historia.

SURA YA 2

Roho Mtakatifu Siku Ya Pentekoste

“Hata ilipotimia Siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja. Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upopo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza *kusema kwa lugha nyingine* [zingine – KJV], *kama Roho alivyowajalia kutamka*. Na walikuwako Yerusalem Wayahudi wakikaa, watu watauwa, *watu wa kila taifa* chini ya mbingu. Basi sauti hii iliposikiwa *makutano walikutanika*, wakashikwa na fadhaa, *kwa kuwa kila mmoja ALIWASIKIA WAKISEMA KWA LUGHA YAKE MWENYEWE*. Wakashangaa wote, wakastaajabu wakiambiana, Tazama, hawa wote wasemao si *Wagalilaya*? Imekuwaje basi *SISI KUSIKIA KILA MTU LUGHA YETU TULIYOZALIWA NAYO*? Waparthi na Wamedi na Waelami, nao wakaao Mesopotamia, Uyahudi na Kapadokia, Ponto na Asia, Frigia na Pamfilia, Misri na pande za Libia [Libya] karibu na Kirene, na wageni watokao Rumi, Wayahudi na Waongofu, Wakrete na Waarabu; *TUNAWASIKIA HAWA WAKISEMA KWA LUGHE ZETU matendo makuu ya Mungu.*” Matendo 2:1-11.

Siku ya Pentekoste Kule Yerusalemu

Hiki ndicho chanzo kikuu kwa utafiti wo wote juu ya kushuka kwa Roho Mtakatifu juu ya kanisa lile la mwanzo, kwa sababu kinaweka *tarehe* kwamba ilikuwa “Siku ya Pentekoste,” kinataja *mahali* kuwa ni “orofani” mjini Yerusalemu (Matendo 1:4,13), na *watu* waliohusika kuwa “jumla ya majina ilipata mia na ishirini” (fungu la 15) pamoja na Mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake Yesu, na wanafunzi wote wa kwanza isipokuwa Yuda (fungu la 13 na la 14).

Kuna mahali pengine pawili palipotajwa katika kitabu cha Matendo. Mahali pamoja ambapo Roho Mtakatifu aliwajia *Wayahudi* na *Mataifa*, wakiwa wote pamoja, na *unenaji wa lugha* ukafuata ni katika ile sura ya 10, mafungu ya 44-46. Mahali pengine ni katika Matendo 19:1-7, ambapo *karama hiyo ya lugha* iliwajia wanaume wale kumi na wawili wa Efeso wakati ubatizo wao katika jina la Yesu ulipochukua nafasi ya ubatizo wao wa Yohana [walibatizwa mara mbili].

Je, Lugha Zilizonenwa Zilijulikana au Hazikujulikana?

Lugha iliyotumika kuelezea Matendo 2:4 inasema kwamba wale walioipokea karama ile ya lugha walisema “kwa lugha nyingine [zingine – KJV],” yaani, walisema kwa lugha zaidi ya zile walizozitumia kwa kawaida kama lugha zao za kuzaliwa nazo. Wakati ule wa Pentekoste walikuwapo “Wayahudi wakikaa, watu watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.” Fungu la 5. Wayahudi wale walikuwa wametawanyika mionganoni mwa mataifa kwa kipindi kirefu sana, na wengi wao hawakuweza kusema tena Kiebrania au Kiaramu. Karama ile ya lugha iliawezesha kutoa hotuba na ushuhuda kuhusu “*matendo makuu ya Mungu*” (fungu la 11) aliyotenda kwa njia ya Yesu wa Nazareti, kiasi kwamba Wayahudi wale waliokuwa si wa nchi ile ya Palestina, yaani, *wahujaji* wale waliokuja katika Mji ule Mtakatifu wa Yerusalemu, waliweza kuelewa yote yaliyosemwa katika lugha za mahali kwao walikotoka.

Ni dhahiri kwamba *lugha zilizonenwa pale ni zile tu zilizojulikana na watu*. Wasikilizaji wale *walishangaa sana* “kwa kuwa kila mmoja aliwasikia wakisema kwa lugha yake mwenyewe.” Matendo 2:6.

“Kila lugha inayojulikana ilikuwa imewakilishwa na wale waliokusanyika pale. Lugha zile mbalimbali zingekuwa kipingamizi kikubwa kwa utangazaji wa injili ile; kwa hiyo *Mungu kwa njia ya mwujiza aliujazia upungufu waliokuwa nao wale mitume*. Roho Mtakatifu aliwafanyia kile ambacho wasingeweza kukipata katika maisha yao yote. *Kuanzia sasa* [wakati ule] wangeweza kuzitangaza mbali kweli zile za injili, *wakisema kwa usahihi lugha za wale waliokuwa wanawahudumia.*” - Ellen G. White, *The Acts of the Apostles* (Matendo ya Mitume), kurasa za 39 na 40.

Katika Matendo 2:6,8,11 ni dhahiri kwamba matangazo yale yaliyounga mkono injili ya Kikristo yalitolewa yote katika lugha zilizokuwa zinajulikana, wala zile kabisa *hazikuwa aina fulani ya kunena maneno kwa msisimko* ambako hakuna mtu ye yeyote aliyelewa kilichosemwa. Roho Mtakatifu alikuwa ameweka ndani ya watu wale *karama ya kunena maneno YANAYOELEWEKA* [aina ya lugha fulani zinazoeleweka kwa watu], hiyo siyo *karama ya kutafsiri lugha* [1 Kor 12:10,11]. Hii ya mwisho *haikuhitajika* pale.

Ishara-ya-Karama ya Kimwujiza Yenye Kuzaa Matunda

Karama hiyo ya *kunena kwa lugha* ni mwujiza wa kushangaza sana, zaidi sana kuliko kule kunena aina fulani ya maneno yasiyoleweka kwa mwanadamu ye yote au kwa malaika. Kumwagwa kwa

Roho Siku ile ya Pentekoste kulikuwa kunatimiza unabii wa Bwana wetu alioutoa katika Marko 16:17: “Na *ishara hizi* zitafuatana na *hao waaminio*; kwa jina langu watatoa pepo; *watasema kwa lugha mpya* [lugha zingine mpya – KJV].

Roho Mtakatifu aliwatumia Wayahudi wale pale Yerusalem kunena na ndugu zao Wayahudi, watauwa, waliowatembelea, lakini ambao *walikuwa hawaamini* kwa kuwawezesha kutumia lugha zao wenyewe ili kuthibitisha ukweli wa injili ya Kristo yule aliyefufuka. Ilikuwa ni tukio la aina yake, ambalo lilifanya iwepo haja ya uthibitisho wa pekee wa aina fulani. Ilikuwa ni ishara kuu kuliko zote ambayo watu wale wangeweza kuipokea, na ushahidi unaoonyesha kufaa kwa ile ishara-ya-karama unaonekana kwa kuangalia matokeo yake. “Nao waliolipokea neno lake [Petro] wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.” Matendo 2:41.

Kuna matumizi sita ya neno hili “isiyojulikana” kuhusiana na “lugha” katika Toleo la Biblia la Mfalme Yakobo (King James Version – KJV) katika 1 Wakorintho 14:2,4,13,14,19,27, lakini katika kila mfano neno hilo limeandikwa kwa herufi-mlazo za italic (italics), kuonyesha kwamba wale waliotafsiri waliweka neno hilo pale kwa kushindwa katika jitihada yao ya kuifafanua maana yake. Ni nyongeza ilioingizwa kwa bahati mbaya. Nyongeza hiyo haionekani katika baadhi ya tafsiri za karibuni zaidi.

Katika Nyumba ya Kornelio Kule Kaisaria

Kule Kaisaria, mji mkuu mmoja wa Kiroma katika Palestina, aliihi afisa mmoja wa Kiroma mwenye uwezo usio wa kawaida. Kornelio alikuwa akida wa kikosi, “mtu *mtauwa*,” aliyejkuwa “*mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote*.” Alikuwa *mkarimu* na mtu *mwenye maombi*. Matendo 10:1-43 isomwe kwa makini kuona jinsi Mungu alivyoshughulika na mtumishi wake Petro kwa kutumia mbinu ili apate kukabiliana na huyo Kornelio Mmataifa, mcha Mungu, na kwa njia ile kuivunjilia mbali chuki yake ya kitaifa isiyo na sababu. Wakati ule ule Mataifa wale waliingizwa kwa njia ya wazi zaidi katika ufalme wa Mungu uliokuwa unaenea kila mahali. Chuki kwa upande wa Wayahudi dhidi ya kuwapokea Mataifa, katika ushirika ule wa Kikristo ililetu shida nyingi katika kanisa lile la mwanzo. Angalia Matendo 11:1-3. Makatazo makali ya Waebrania wale dhidi ya wale wasiokuwa Wayahudi, kwa ukaidi yalibaki miyononi mwa Wakristo wale wa kwanza na Kiebrania kiasi kwamba ulihitajika ushuhuda wenye nguvu kabisa wa kushuka kwa Roho Mtakatifu juu ya Mataifa wale ili kufutilia mbali chuki ile. Jambo hilo litaonekana katika Matendo 11:15-18.

Lugha iliyonenwa katika Matendo 10:44-48 *inafanana* na ile iliyonenwa katika Matendo 2. Tofauti iko katika ukweli kwamba wale Wakristo Waebrania wenzake na Petro, wakiwa hawapendi kuwaingiza Mataifa wale katika ushirika wa Kikristo, sasa wanaona Roho Mtakatifu akitenda kazi yake kupitia kwa Kornelio na wenzake, *wakimsifu Mungu* kwa lugha ambazo hawakuzaliwa nazo:

“Na wale waliotahiriwa, walioamini, *wakashangaa*, watu wote waliokuja pamoja na Petro, *kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu*.” Matendo 10:45.

Uthibitisho unaoonyesha kwamba ishara hiyo kwa Wayahudi wale wasioamini na kwa Mataifa wanaoamini ilikuwa katika lugha zinazoleweka kwa wanadamu, wala sio maneno yasiyojulikana yaliyosemwa kwa msisimko, unaonekana wazi katika Matendo 11:15. Pale Petro alipokuwa amekwisha kurudi Yerusalem, na kutoa taarifa ya tukio lile la Kornelio linalowavutia watu wengi kwa ndugu zake wenye kutaka shari [wagomvi] ambao wasingependa kuwa na Mataifa katika jamii yao ile nzuri. Aliwaambia waziwazi maneno haya: “Ikawa nilipoanza kunena, Roho Mtakatifu akawashukia *kama alivyotushukia sisi mwanzo*.” Matendo 11:15. Ni dhahiri kwamba “mwanzo” humaanisha ile Siku ya Pentekoste, wakati lugha zile zilikuwa “ngeni” kwa wanenaji, lakini zilijulikana kwa waskilizaji.

Ushahidi kwa Wayahudi na Mataifa

Siku ile ya Pentekoste lengo kubwa la kipawa kile cha Mungu lilikuwa ni kuwaongoa watu wake Waisraeli, lakini kwa Kornelio na nyumba yake jamii ile ilipanuka na kuwajumuisha Mataifa. Tunaweza kuwazia vema shida waliyoipata ndugu zake Wakristo wale wa Yudea amba walijihesabia haki wenyewe walipomshambulia Petro na wenzake baada ya tukio lile la kusisimua sana lililotokea katika nyumba ya Kornelio, na kusema: “Uliingia kwa watu wasiotahiriwa ukala nao.” Matendo 11:3.

Kwa kulandana vema na hali ile, sisi twaweza kuwazia hali ile ya kutokuamini ilivyokuwa ikigeuka na kuwa furaha takatifu wakati Petro alipo “anza kuwaeleza kwa taratibu jambo lile tangu mwanzo.” Fungu la 4, KJV. Kama wale rafiki zake Petro katika nyumba ile ya Kornelio amba walishangaa “kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu” (Matendo 10:45), ndugu wale wa Yerusalem waliochukia bila sababu walishangaa sana. “Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu, wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata Mataifa nao toba liletalo uzima.” Matendo 11:18.

Hakuna ushahidi wo wote katika matukio hayo unaonyesha kwamba Roho Mtakatifu na karama ile ya lugha kwa maana yo yote ile ilikuwa tofauti na yale mambo yaliyowapata wao Siku ile ya Pentekoste. Palikuwa na sababu nzuri kwa nini familia ya Kornelio inene kwa lugha, kwa maana *vinginevyo wenzake Petro wasingewakubali watu wale wa Mataifa kama ni wapokeaji halali wa uweza wa Roho Mtakatifu*. Hiyo tena ilikuwa ni ishara-ya-karama nyingine, ikiwashuhudia Wakristo wale wa Kiebrania waliokuwa hawapendi kwamba kuanzia wakati ule kwenda mbele kanisa la Kristo liwachukue watu wa kila taifa chini ya mbingu [Mdo. 10:34,35].

Ni lugha gani hasa zilizosemwa kwa njia ya kipawa kile katika nyumba ile ya Kornelio hazitajwi hapo. Lakini, je, haiyamkiniki kwamba wacha Mungu wale wa Mataifa walimsifu Mungu katika lugha ile ile ya ndugu wale sita wa Kiebrania wasioamini - kwa Kiaramu, ama kwa Kiebrania?

Waongofu wa Yohana Mbatizaji pale Efeso *Matendo 19:1-7*

Tukio linalofuata linatuleta sisi kwenye mkabala ule kati ya waongofu wale kumi na wawili wa Yohana, amba walifundishwa na Apolo, Myahudi wa Iskanderia, na mtume Paulo pale Efeso. Mtume yule mkuu kwa sasa alikuwa na cheo cha kuwa “mtume kwa Mataifa.” Alikuwa ameahidi kurudi katika mji ule wa Efeso (Matendo 18:21), naye alipofanya vile aliwakuta “wanafunzi kadha wa kadha huko.”

Kama alivyokuwa mwalimu wao Apolo, ujuzi wao wa mafundisho ya Kikristo bila shaka ulikuwa na upungufu kama linavyodhihirisha swali hili: “Je! mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini? Wakamjibu, La, hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia.” Matendo 19:2.

Watu wale walionekana kana kwamba wanajua kidogo zaidi ya yale mafundisho ya toba aliyoleta ameyatoa Yohana Mbatizaji ambayo yaliletwa kwao na Apolo. Ni dhahiri kwamba Paulo alilichukulia jambo lile kuwa ni la kweli kwamba kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ni lazima awe amekwisha kumpokea Roho Mtakatifu. Katika kuongoka ko kote kwa kweli Roho Mtakatifu hufanya mwujiza kwa kumwongoza mwenye dhambi katika maisha yale ya “haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu.” Warumi 14:17.

Wakiwa wamepata mafunzo yao kwa sehemu tu, watu wale walikuwa wamebatizwa “kwa ubatizo wa Yohana.” Paulo aliendelea kuwapa mafunzo maalum na kuwaingiza katika imani ya Kikristo. Hotuba yake haijatolewa yote hapo, lakini ni dhahiri kwamba Paulo hakuwabatiza [tena] bila kuwapa

mafundisho maalum ya Kikristo. Kilele cha mafundisho ya Paulo kimefanuliwa kwa maneno haya: "Yohana alibatiza kwa ubatizo wa toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani, Yesu." Matendo 19:4.

Ni dhahiri kwamba huko kumweka Kristo Mkombozi kuwa kitovu ndiyo hatua ya msingi katika kuongoka kwa watu wale, sio zile karama za lugha zilizofuata baadaye. Waongofu wale wa Apolo walikuwa katika "nusu ya nyumba," kama mtu fulani alivyosema, "katikati ya Dini ile ya Kiyahudi na Ukristo," na Paulo aliwaongoza njia yote iliyobaki na kuwabatiza katika jina lake Kristo. Kwake [Paulo] kulikuwa na "Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja" tu. Waefeso 4:5.

"Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza *kunena kwa lugha*, na kutabiri." Matendo 19:6.

Luka anatumia mahali hapo neno la "*glossa*" anapoandika kumbukumbu yake ya karama hiyo ya lugha, neno lile lile lililotumika katika Matendo 2:4,11 na 10:46, wala hakuna sababu yo yote ya kutoa maana yo yote nyingine zaidi ya hiyo ya lugha au ndimi zile zinazojulikana na watu. Kulikuwa ni kumwagwa kwingine kwa Roho Mtakatifu kama kule kwa Pentekoste. Kulileta matokeo kwa Wayahudi wale, kama katika siku ile ya Pentekoste, lakini wakati ule mahali penyewe palikuwa ni kituo cha shughuli za watu wa Mataifa. Kwa hiyo, Wayahudi na Mataifa, walishangaa sana na kuguswa sana moyoni mwao na kumletea Mungu utukufu. Walipewa uwezo wa kutangaza injili katika Efeso na mahali penginepo pote kwa kipawa hicho.

Karama ya Lugha Ilienea kwa Kiasi Gani?

Hajakosa kuona msomaji mwenye kufikiri ya kwamba vifungu vyta maneno hivyo vitatu ambavyo tumejifunza katika kitabu cha Matendo (Sura ya 2:4; 10:46; 19:6) ni matukio matatu ya kuvutia sana ambayo yalitokea katika kipindi fulani cha wakati. Hakuna ushahidi mwingine wo wote unaoonyesha kwamba karama hiyo ya lugha ilikuwa imeenea mahali pengi, au kwamba ilikuwa ni uzoefu wa watu wote katika kanisa lile la kwanza. Tutamruhusu S. Lewis Johnson, Jr., kutufanya muhtasari wake:

"Karama ya lugha kulingana na Matendo ilikuwa ni karama iliyowawezesha wapokeaji wake kunena kwa ndimi au lugha zinazojulikana, kwa nyakati fulani zilizopangwa na Roho Mtakatifu ili kuthibitisha ukweli wa ujumbe uliotolewa na kanisa lile la kwanza mbele ya Wayahudi. Kwamba hawakuwa nayo waumini wote katika kanisa lile la kwanza ni dhahiri kutokeana na kutokeana kwake mara chache mno katika kipindi kile cha matendo, na kutokeana na semi maalum katika zile Nyaraka (linganisha na 1 Kor. 12:30; Ebr. 2:3,4)." - *Biblioteca Sacra*, Oktoba, 1963.

Hitimisho lo lote lisemalo kwamba karama ya lugha ilikuwa kwa watu wote katika kanisa lile la kwanza haliungwi mkono na kitabu cha Matendo. Wala sisi tusingefikia hitimisho kwamba matukio yale machache yaliyotajwa ya kupokea "lugha" yalimaanisha kwamba wao walipata ongezeko la nguvu za kiroho zaidi ya zile zilizoonekana ndani ya waumini wengine.

"Kando ya ushuhuda wao ule wa mwanzo na 'unabii,' je! kuna ushahidi wo wote wa Biblia unaoonyesha kwamba waliokuwa katika nyumba ya Kornelio au Waefeso wale kumi na wawili walikuwa na uwezo au walikuwa na manufaa ndani ya kanisa lile la Kristo kuliko alivyokuwa yule Dorka au Lidia? Hakika kila Mkristo mnyofu wa moyo atakubali kwamba hakuna ushahidi wo wote kama huo katika Biblia." - H. J. Stolee, *Speaking in Tongues*, ukurasa wa 44.

Mifano hiyo ya karama ya lugha iliyandikwa na kuwekwa katika kumbukumbu katika kitabu hicho cha Matendo, kama tulivyokwisha kuona, haileti utata mkubwa uwao wote. Lakini tutagundua mambo yaliyo na utata mwangi zaidi katika Waraka ule wa Kwanza kwa Wakorintho. Ni dhahiri kwamba makanisa yale ya Kikorintho yalikuwa na matatizo ya aina nyingi, yakiwamo na matatizo ya

kutokuwa na utaratibu kanisani ambayo yalisababishwa na kunena kwa lugha, kama tutakavyoona hivi sasa.

SURA YA 3

Ushahidi Mwingine wa Agano Jipyä

“Mjazwe Roho”

Endapo karama hiyo, kama wasemavyo baadhi ya washabiki wa “kunena kwa lugha,” wangekuwa nayo kwa kawaida katika maisha yao Wakristo wote Waliojazwa-na-Roho, basi, tuna vifungu fulani fulani vinavyoleta ugumu katika Agano Jipyä ambavyo vinapasa kufafanuliwa. Hapa hatuna budi kuviangalia baadhi yake kwa kifupi.

Rafiki zetu wa Kipentekoste wanapozungumza juu ya “kungoja” [kukaakaa] wao wanaona kwamba Yesu aliposema, “kaeni,... hata mvikwe uwezo utokao juu” (Luka 24:49), alimaanisha kukaakaa, au kungoja ili Roho aje. Hivyo waumini wao leo wanaamua kukaa katika maombi, sifa, na ibada katika mikutano yao inayochukua muda mrefu sana mpaka hapo kitu fulani kinapotokea kwao - na mara kwa mara kitu hicho hutokea usiku sana. Kwa maneno mengine, muumini anaamua kwamba ataitafuta na kuipata karama hiyo ya lugha. Ni dhahiri kwamba maneno hayo ya Bwana wetu yalikataza kuhubiri injili kila mahali mpaka wanafunzi wale walipotayarishwa na Roho Mtakatifu, si lazima iwe kwa njia ile karama ya lugha.

Ni kweli kwamba katika Waefeso 5:18 mtume Paulo anasema, “mjazwe Roho,” lakini hakuna hata neno moja katika fungu hilo, wala katika sura hiyo yote liwezalo kuhalalisha fungu hilo kumaanisha, “Amua mawazoni mwako kutafuta, kungojea, kufanya kazi, ili upokee Roho, nawe utanena kwa lugha.” Wala hata kule “kunena kwa lugha” hakujagusiwa hapo kuwa ni kitu anachopata kila muumini katika maisha yake.

Ni kweli kwamba katika Waefeso 5:18 mtume Paulo anasema, “mjazwe Roho,” lakini hakuna hata neno moja katika fungu hilo, wala katika sura hiyo yote liwezalo kulihalalisha fungu hilo kumaanisha, “Amua mawazoni mwako kutafuta, kungojea, kufanya kazi, ili upate kupokea Roho, nawe utanena kwa lugha.” Wala hata kule “kunena kwa lugha” hakujagusiwa hapo kuwa ni kitu anachopata *kila muumini* katika maisha yake.

Zaidi ya hayo, kukitupia jicho kwa haraka kitabu kile cha Waefeso, sura ya tano na ya sita, kutatuonyesha sisi kwamba Paulo anaongea juu ya muumini ku “enenda katika *upendo*” (Efe. 5:2), au juu ya maisha ya muumini huyo ya kila siku ndani ya Kristo yahusuyo usafi wa maadili, mwenendo mzuri, kuepuka “matendo ya giza,” kuwa macho dhidi ya hatari za nyakati hizi, kutotumia kileo, kuwa na shukrani, kuwa na ndoa yenyе furaha, kufanya kazi kama viungo vya mwili wa Kristo, kuwaheshimu wazazi, na kwa jumla kusimama bila hofu katika kumshuhudia Mungu. Hakuna neno lo lote linalosemwa juu ya “kunena kwa lugha” kwa waumini kama hao. Lakini kulingana na umuhimu wake imenenwa hivi: “Kwa kuwa *tunda la Roho* ni katika wema wote na haki na kweli.” Waefeso 5:9.

Linapokuja suala la kuamua kujipatia karama hiyo ya kunena kwa lugha, tunaukuta usemi huu dhahiri unaohusu mamlaka ya Mungu kulingana na mapenzi yake: “Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, *apendavyo Roho yeye yule*; mwingine imani

katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, AKIMGAWIA KILA MTU PEKE YAKE KAMA APENDAVYO YEYE [ROHO].” 1 Wakorintho 12:8-11.

Maneno ya mwisho huonyesha kwamba kuwapo kwa karama yo yote ya Roho Mtakatifu kunategemea *maamuzi ya Mungu*, hakutegemei mapenzi ya mwanadamu. Tafsiri nyingine za kifungu hicho cha maneno zinasema: “Anayegawa kwa kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.” R.S.V. “Anayegawa kwa kila mtu, apendavyo yeye.” Phillips. “Azigawaye moja moja kwa kila mtu apendavyo yeye.” N.E.B.

Mungu anatuweka sisi kama viungo katika mwili wake, yaani, kanisa lake, na kwa hekima yake kutupa sisi uwezo wa karama za kiroho za aina mbalimbali tofauti kwa ajili ya *kulijenga kanisa zima*. “Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili *kama alivyonaka*.” 1 Wakorintho 12:18.

Maana ya Kuwa Kimya

Kitabu cha Matendo kimeitwa “Matendo ya Roho Mtakatifu” na baadhi ya wataalam wa Biblia kwa sababu imeandikwa humo kwamba kuihubiri injili ya Kristo ulimwenguni kote ni kazi ya Roho Mtakatifu kuititia kwa wanaume na wanawake waliojitoa wakf. Sisi tungetazamia kwamba kitabu hiki, zaidi ya vitabu vingine vyote vya Agano Jipya, kingeweza kutoa jibu dhahiri kwa swali lisemalo, je! huko “kunena kwa lugha” kuweze kufikiriwa kuwa ni jambo la kawaida katika maisha ya [kila] Mkristo.

Tunachokiona humo ni kwamba neno hili la *Kigiriki glossa* - ndimi, lugha - limetumika mara sita katika kitabu cha Matendo. Mawili kati ya mafungu hayo (Matendo 2:3,26) hayana uhusiano wo wote na karama hiyo ya lugha, kiasi kwamba ni mara nne tu katika sura zile ishirini na nane za kitabu hicho ilimotajwa karama hiyo (Matendo 2:4,11; 10:46; 19:6).

Mawili ya kwanza kati ya mafungu hayo manne yanataja tukio lile lile - Pentekoste. Kwa hiyo kwa zaidi sana ni *matukio matatu tu yaliyoandikwa* katika kitabu hicho kinachosisimua cha Matendo ambacho kina historia ya mwanzo ya kanisa. (Kwa kweli, hakuna kumbukumbu zo zote za karama hiyo ya lugha katika Injili zote nne.)

Lakini shida kubwa ya kupatikana kwa ushahidi wo wote ina kina kirefu sana kuliko hicho. Palikuwa na *waongofu 3,000* Siku ile ya Pentekoste. Angalia Matendo 2:41,42. Katika Matendo 2:47 wengine wanatajwa: “Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.” Halafu katika Matendo 4:4 waongofu karibu 5,000 wanatajwa. Zaidi ya hapo tulipofikia, inaelezwa hivi katika Matendo 6:7: “Neno la Mungu likaenea; na hesabu ya wanafunzi ikazidi sana katika Yerusalem; jamii kubwa ya makuhani wakaitii ile Imani.”

Je! katika ongezeko hilo kubwa sana la watu walioingia katika ushirika wa kanisa lile la kwanza alikuwamo mtu ye yote aliye kuwa Mkristo ambaye alifurahia “kunena kwa lugha” kama sehemu ya maisha yake ya kawaida? *Pana ukimya juu ya jambo hilo*. Walikuwa na kipawa cha Roho Mtakatifu juu yao, lakini *hawakuwa na karama hiyo ya lugha* kwa kadiri kumbukumbu hiyo inavyoeleza.

Walakini, tunasoma kwamba idadi kubwa ya waumini wale “wote wakajaa Roho Mtakatifu, *wakanena neno la Mungu kwa ujasiri*.” Matendo 4:31. Huo hauwezi kufikiriwa kuwa ni mfano wa moja kwa moja, kama tunavyotumaini, endapo sisi tunasema kwamba *kile kinachotakiwa leo ni ujasiri mwingi ulio mtakatifu wa kuitangaza Injili ya wokovu kwa ulimwengu* huu unaoangamia, kuliko kufurahia kuwa na maonyesho mengi zaidi ya misisimko ndani ya makaniisa yetu au nyumbani mwetu.

Msomaji aliye mwangalifu kuchunguza miujiza ya kila aina, na matukio mengine yaliyokuwa yanavutia macho sana katika kitabu hicho cha Matendo, ataona kwamba Roho Mtakatifu alikuwa

anatenda kazi yake kwa uweza mkuu. Hata hivyo, hakuna uzoefu wa kunena kwa lugha ulioandikwa [kuhusiana na matukio hayo]. Angalia Matendo 3:1-11; 6:3-8; 9:36-42; 16:25-34, na kadhalika.

Tena, hebu chukua wahusika waliojitokeza sana katika kitabu hicho cha Matendo, mbali na Paulo na Petro. Hao, kwa mfano, walikuwa ni Stefano, Yakobo, Agabo, Simeoni, Filipo, Sila, Timotheo, Barnaba, Lidia, Dorka, Krispo, Apolo, Akwila, Prisila, kuwataja wachache tu. Hao walifanya kazi kubwa kwa ajili ya Mungu, lakini hatujui habari yo yote kuhusu uzoefu wao wa “kunena kwa lugha,” zile zinazojulikana au zile zisizojulikana, ndani ya mmojawapo miongoni mwao. Lingekuwa ni jambo la kufurahisha na kusisimua sana jinsi gani katika kitabu hicho cha Matendo kama “kunena kwa lugha” kungekuwa ndani ya kila muumini! Lakini ni dhahiri kwamba jambo hilo halikuwamo katika kusudi la Mungu kwao. Don W. Hills amesema, “Ni tabia ya kibinadamu kutamani kuyakuza sana mambo yale ya kusisimua. Kitabu cha Matendo kimefanikiwa kuyakwepa hayo.” - *What Can Tongues Do For You?* (Kunena kwa Lugha Kwaweza Kukutendea Nini Wewe?), ukurasa wa 28.

Kando ya ushahidi tulioueleza kutoka katika kitabu hicho cha Matendo na Waraka wa Kwanza kwa Wakorintho, hakuna jambo jingine zaidi lililoandikwa katika kumbukumbu za Agano Jipyka kuhusu karama hiyo ya lugha. Jambo hilo ni la maana sana. Lakini basi, isije ikafikiriwa kwamba huo ni ushahidi ulio na mwelekeo wa kanusha tu, yatupasa kukumbuka semi zile nyingi zinazohusu haja ya kuwa na Roho Mtakatifu katika maisha ya kila muumini. Asiwepo mtu ye yote anayedharau umuhimu wa Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo.

Umuhimu wa Roho Mtakatifu

Yesu alimwambia Nikodemo: “Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezo kuuingia ufalme wa Mungu.” Yohana 3:5. Huko ni kutajwa kwa ku“zaliwa mara ya pili,” kama ilivyoelezwa katika fungu la 3; na katika fungu lile la 8 uzoefu huo unasemekana kwamba ni vigumu kuweza kuueleza ulivyo. Ni badiliko la kimwujiza linalofanyika ndani ya mtu yule anayeziungama dhambi zake na ambaye anatamani ku“huish[wa],” au kuwa na uzima ndani ya Kristo. Waefeso 2:5.

Kwa watu kama hao walioongoka, Yesu, alipoondoka duniani, aliwaahidi kuwapo daima kwa “huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu.” Yohana 14:26. Kusudi la utume wa Roho Mtakatifu lilikuwa ni kuwafanya waumini watambue kuwapo kwake Kristo, kumtukuza Kristo katika maisha ya Mkristo, kuwafundisha, na kuwaongoza katika njia za ile kweli. Angalia Yohana 16:7,8,13,14. Roho Mtakatifu alipaswa kumfunulia muumini “hata mafumbo ya Mungu” (1 Wakorintho 2:10), kumtia muhuri ili awe mali yake Mungu (Waefeso 1:13), na kuwa uthibitisho wa kuwako kwake Kristo ndani ya kanisa lake “hata ukamilifu wa dahari [mwisho wa dunia].” Mathayo 28:20, KJV. Angalia pia Yohana 14:21-23.

Kwa hiyo, waumini ni lazima wawe wanaume na wanawake waliojazwa Roho. Warumi 8:9. Lakini basi, hakuna mahali po pote katika kumbukumbu hizo pamoa na nyinginezo nyingi zinazohusu kazi ya Roho Mtakatifu tunapopata hata dokezo moja dogo sana kuonyesha kwamba aina yo yote ya karama ya lugha ingekuwa ndilo tunda au kipawa cha Roho Mtakatifu ndani ya maisha ya *kila* muumini. Badala yake, imeelezwa kwa wazi kabisa kwamba “tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi.” Wagalatia 5:22,23. Wakristo wanaoonyesha tunda lo lote katika hayo katika maisha yao walitakiwa kufurahia “haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu.” Warumi 14:17. Msomaji anawenza kuangalia na kuzingatia *matunda* ya Roho katika Wagalatia 5:22,23 na kuyalinganisha na *karama* za aina tisa za Roho zinazopatikana katika 1 Wakorintho 12:28, na kuona kwamba ile lugha inatolewa mwishoni mwa kila orodha, ingawa umuhimu usiostahili usingepaswa kuwekwa juu yake kwa kuzingatia ukweli huo.

Kuna mafundisho mengi sana katika Agano Jipyka kuhusu kazi zake huyo Roho Mtakatifu; lakini, pamoa na tofauti chache mno zinazoonekana wazi ambazo tumekwisha kuzitaja, kuna habari kidogo

sana kuhusu hiyo karama ya lugha. Wakristo wale wa mwanzo “wakaenda huko na hiko *wakilihubiri neno*” (Mdo. 8:4), walitoa ushuhuda wao juu ya Kristo “mpaka kuuawa”; walikabiliwa na uhasama mkali sana karibu kila mahali walikokwenda; wali“upindua ulimwengu” (Matendo 17:6) - mambo yote hayo walifanya kwa kupewa uwezo na Roho wa Mungu. Lakini wachache mno, wachache mno kabisa, na hao wakiwa ni idadi inayozidi kupungua, walichaguliwa na Mungu kuitumia karama hiyo ya lugha. Jambo hilo linatia mkazo fulani juu ya uwiano wa kutokuwapo umuhimu wa karama hiyo baada ya kutumika kwake mwanzoni katika matukio yale machache.

Endapo tungewuliza Mtume yule mkuu Paulo kwamba tamaa yake ilikuwa ni nini kwa muumini, yeze angeweza kusema: “Ufuateeni *upendo*, na kutaka sana *karama za rohoni*, lakini zaidi kwamba *mpate kuhutubu*.” 1 Wakorintho 14:1-5, KJV. Je, ingekuwa ni kuipanua sana hoja hiyo juu ya uwiano usio na maana kuhusu karama hiyo ya lugha iliyoleta usumbufu mwangi katika makanisa yale ya Kikorintho?

Si kila mmoja wetu ambaye angeweza kunena kwa lugha, kwa mujibu wa Paulo. Hata wale waliotakiwa “kutaka sana karama za rohoni” walishauriwa hivi: “Hata hivyo nawaonyesha *njia iliyo bora*.” 1 Wakorintho 12:31. Kuwapenda watu wote na kuhubiri bila kuona fahari katika kitu cho chote ila msalaba wake Kristo - hiyo ndiyo njia iliyo bora. Wagalatia 6:14.

SURA YA 4

Karama ya Lugha Kule Korintho

Hali ya Kiroho Pale Korintho

Mtume Paulo alitumia sehemu kubwa ya Waraka wake wa Kwanza kwa Wakorintho (sura ya 12 hadi ya 14) kuzungumzia karama za Roho Mtakatifu. Mengi mionganini mwa mashauri yake yalishughulikia suala hilo la karama ya lugha.

Wakati Yesu anapaa “akawapa wanadamu vipawa [karama].” Waefeso 4:8. Karama hizo zimeorodheshwa kama *mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu*. Fungu la 11. Kusudi la kutoa vipawa [karama] hivyo vya kiroho limeelezwa katika fungu la 12. “Kwa kusudi la *kuwakamilisha watakatifu*, hata kazi ya *huduma itendeke*, mwili wa Kristo [kanisa] ujengwe.”

Hali ya kiroho ya Kanisa lile la Korintho ilikuwa imeshuka chini. Jambo hilo linaonekana karibu katika Waraka wote wa kwanza wa Paulo, wakati huo Korintho ulikuwa ni mji wenye mwonekano wa kidunia [kipagani], mji wa kistaarabu, wenye shughuli za kibiashara zilizowaleta wachuuzi na mabaharia toka mashariki na magharibi. Ulikuwa ni makao ya hekalu la Afrodite (Aphrodite), Mungu

wa ashiki [uasherati] na uzuri, ulikuwa na makuhani wa kike makahaba [malaya] 1,000 wakiendesha ibada zao za uasherati juu ya Acro-Corinthus. Walakini, mji ule ulikuwa na uadilifu mzuri wa bandia. Lilikuwa ni jambo la kawaida kwa wote kusema kwamba mwanaume mwasherati sana mwenye maadili mema kwa nje alikuwa amegeuka na kuwa Mkorintho” - usimi ambao bado unatumika kule mpaka leo.

Kanisa lile la Kikorintho liliathirika kutokana na mazingira yake. Lilikuwa na vipawa, lakini lilikuwa si la kiroho. Lilikuwa na majivuno, na kuwa na mwelekeo wa kulidharau Neno la Mungu. Mafungu kama 1 Wakorintho 4:6-10,18; 5:2; 14:37, na sura ya 8 na ya 12, yanaonyesha picha ya kanisa lile lililokuwa na makuu na lenye kujitosheleza lenyewe. Pia lilikuwa ni kanisa lenye fitina (1 Wakorintho 1:11), na zinaa ya kuchukiza mno ilikuwamo katika safu zake. 1 Wakorintho 5:1.

Karama za Kiroho Korintho katika Hali Isiyo ya Kawaida

Ilikuwa ni katika kanisa kama hilo ya kwamba karama ile ya lugha ilikuja kama mojawapo mionganoni mwa karama nyingi za kiroho. 1 Wakorintho 12:1-10. Karama hizo tisa zilikuwa *hekima, maarifa, imani, karama za kuponya, matendo ya miujiza, unabii, kupambanua roho, aina za lugha, tafsiri za lugha*. Fungu la 8-10. Juu ya karama hizo zote, karama ya [kunena kwa] lugha inaonekana kana kwamba ndiyo karama ambayo kwayo Kanisa la Korintho liliona fahari. Bila shaka ilizidi kiasi hata ikabidi Paulo ajitahidi sana kuirekebisha.

Katika 1 Wakorintho 12:3, KJV, mtume huyo anasema hivi: “Kwa hiyo nawaarifu, ya kwamba *hakuna mtu anenaye katika Roho wa Mungu*, anayemwita Yesu kuwa amelaaniwa.”

Maneno haya yenyе herufi za mlazo - *en pneumati theou lalon* - yana uhusiano wa karibu sana na maneno yake katika 1 Wakorintho 14:2, yaliyotumika kuhusiana na kunena kwa lugha. Linaonekana kana kwamba ni jambo lisilosadikika kwamba mtu anayejidai kwamba ananena kwa lugha angeweza kumlaani Yesu (neno hili “amelaaniwa” linatokana na neno la Kigiriki *anathema*), hata hivyo, ni dhahiri kwamba lugha ya kushtua sana kama hiyo ilitumika, labda na wapagani waliotumia karama hiyo mbele ya waongofu wapya wa Kikristo kwa unafiki wao wa kujifanya wanayo karama ya kudhania-dhania tu ya kunena kwa lugha.

Kulikuwa na mambo mengine yaliyokuwa yamevuka mipaka yake ambayo yalionekana katika kanisa hilo. Wanawake waliamriwa “wanyamaze katika kanisa” [1 Kor. 14:34], si kwa sababu lilikuwa ni kosa kwao kushiriki katika maombi na kumsifu Mungu (angalia 1 Wakorintho 11:13), bali kwa sababu zamani ni dhahiri kwamba wanawake wale wa kipagani walikuwa wasemaji mno wasio na haya.

Ukweli ni kwamba kanisa la Kikristo kwa wakati ule lilikuwa halijaweka mfumo na taratibu za kuendesha ibada. Hivyo waongofu waliotoka kwenye upagani walikuwa hawajazoea kufanya “mambo yote ... kwa uzuri na utaratibu.” 1 Wakorintho 14:40. Hata Meza Takatifu ya Bwana iligeuka na kuwa dhihaka ya kumstahi Mungu kwa shamrashamra [kelele na vifijo vyia sherehe] zao na ulevi. 1 Wakorintho 11:20-22.

Katika mazingira kama hayo ikaja ile karama ya lugha. Ni wazi kwamba walikuwamo watu ambao walikuwa wanyofu wa moyo na wenye vipawa katika makanisa yale ya Kikorintho, vinginevyo, zisingetokea ndani yake karama zile nyingine za kweli. Ilikuwa ni karama isiyo ya kawaida [ya ajabu-ajabu] na katika mazingira yasiyo ya kawaida. Sasa yatupasa kulichunguza suala la kunena kwa lugha katika mazingira ya eneo lile kwa undani zaidi.

Paulo na Karama ya Lugha Pale Korintho

Mtume Paulo hapo hajaribu kusifu au kuikuza sana karama ya kunena kwa lugha ikilinganishwa na karama zile nyingine. Kimsingi anawashauri Wakristo hao wenyе haja ya karama hiyo ili wapate kujizoeza *upendo*: “Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina *upendo*, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao.” 1 Wakorintho 13:1.

Hizo “lugha za wanadamu na za malaika” kwa kweli ni usemi unaotumika hapo kutilia mkazo *upendo* kama ndicho kipawa cha maana sana kuliko kinginecho chote. Mafungu matatu ya kwanza ya sura hiyo yanatilia mkazo umuhimu usio na mipaka wa kuwa na upendo huo.

Katika nusu ya mwisho ya sura hiyo ya upendo (fungu la 8-18) usemi unaovutia sana umetolewa kuhusu tabia ya kudumu ya upendo huo, kama ulinganifu huu unavyoonyesha:

1. Upendo - haupungui neno wakati wo wote.
2. Unabii - utabatilika.
3. Lugha - zitakoma.
4. Maarifa - yatabatilika.

Hivyo mkazo wa kwanza uko katika hali ya kuwapo kwa lugha kwa muda unaopita, sio juu ya kuzipita karama zile nyingine zote za Roho. Yaonekana dhahiri kwamba palikuwa na mkazo unaozidi kiasi kuhusu lugha pale Korintho. Mkristo mwenye karama nyingineyo yote katika karama zile za rohoni si kwamba ana nguvu kidogo, au ni duni machoni pa Mungu kuliko yule ambaye ndani yake “karama ya lugha” inajionyesha zaidi. Kwa thamani yake hapo, tunaona kwamba “lugha” imetajwa ya pili toka mwisho katika orodha zile mbili za karama hizo zilizotolewa katika 1 Wakorintho 12:8-10,28-30. Kama tunalazimika kusema juu ya ubora, basi, upendo wa Mungu kama kipawa kitokacho kwa Mungu ni karama ya kiroho inayozipita zote. Mtu anashangaa kwamba endapo karama hiyo kuu kuliko zote [upendo] ingeonekana ndani ya idadi kubwa ya Wakristo wale, je! hivi kungekuwa na kung’ang’ania na kutamani sana karama ile ya kujionyesha sana ya lugha! Endapo wangekuwa na upendo mwangi zaidi, basi, bila shaka pangekuwa na nguvu ya Mungu nyingi zaidi katika kanisa lile kwa ajili ya kuyaboresha au kuyatatua matatizo yaliyomo katika dunia hii na kwa ajili ya ushuhuda wa Kikristo kwa ulmwengu mzima.

Karama ya lugha katika kitabu kile cha Matendo ilitambuliwa kuwa ni uwezo wa Mungu usio wa kawaida aliowapa kwa tukio la pekee, wala haikuleta machafuko yo yote au fitana mionganini mwa waumini wale. Walakini, karama hiyo ya lugha pale Korintho kwa hakika ililetu matatizo ndani ya kanisa lile, na baadhi ya matatizo hayo bado yanaleta mkanganyiko [mfadhaiko] hata leo hii.

Pale karama ya lugha iliambatana na karama ya ‘tafsiri ya lugha’ 1 Wakorintho 12:10. Je! hiyo inamaanisha tafsiri ya lugha ya nchi nyingine? Kama ndivyo, basi, hiyo inafanana na hali ilivyokuwa wakati wa Pentekoste. Au je! hiyo inamaanisha lugha ya Roho, inayojulikana tu na Mungu, ambaye kwa ajili hiyo anampa mshiriki mwagine wa kanisa tafsiri yake?

Katika 1 Wakorintho 14:2,4,13,14,19,27 neno “isiyojulikana” limeachwa, lakini hilo halitatui tatizo lenyewe lililokuwapo tunapoangalia sehemu ya kwanza ya fungu la 2 (kwa Kiswahili): “Maana ye ye anenaye kwa lugha hasemi na watu, bali husema na Mungu; maana hakuna asikiaye [anayemwelewa]; lakini anena mambo ya siri katika roho yake [katika Roho – KJV].

Jambo hilo limewafanya wengi kufikia hitimisho kwamba iko *lugha ya siri ya Roho* ambayo hakuna mwagine ye yote awezaye kuielewa, isipokuwa yule tu anayeipokea karama hiyo. Kwa hiyo hakuna haja ya kuwa na mtafsiri [mkalimani] ye yote, na Mungu hutukuzwa. Walakini, Paulo, anaonekana kana kwamba anatoa jibu kwa jambo hilo kwa kusema hivi: “Vivyo hivyo na ninyi, *msipotoa kwa ulimi neno lililo dhahiri*, neno lile linenwalo *litajulikanaje?* Maana *mtakuwa mkinena hewani tu*. Kisha anaendelea kuondoa mkazo wake juu ya “lugha” kwa kusema, “kwa kuwa mnatamani sana kuwa watu wenyе karama za roho, *takeni kwamba mzidi kuwa nazo ili KULIJENGA KANISA*.” Fungu la 12.

Mwonekano Mwingine wa Karama za Roho Pale Korintho

Paulo aliguswa sana kuona ukosefu wa kujengana katika baadhi ya taratibu za ibada za kanisa lile la Korintho. Hivyo katika 1 Wakorintho 14:26 twasoma maneno haya: “Mkutanapo pamoja, *kila mmoja ana zaburi, ana fundisho, ana ufunuo [unabii], ana lugha, ana tafsiri.* **MAMBO YOTE NA YATENDEKE KWA KUSUDI LA KUJENGA.**”

Wakorintho wale wenye mihemuko [misisimko] ya ghafula, bila kupata msingi wa mafundisho ya Kiebrania na kukosa kuwa na taratibu za ibada zeny kicho, walitamani sana kushiriki katika huduma za kanisa. Wengine walipenda sana kuimba nyimbo (zaburi) katika ibada, wengine walikuwa na kipaji cha kufundisha, na bado wengine walitaka kutoa maarifa fulani waliyojisikia kuwa walipokea kutoka kwa Mungu, na lugha na tafsiri zake pia zilijitokeza sana sana. Wakorintho wale walikuwa wanatamani sana, walikuwa na fitina, na mara nyingi walitenda mambo yao kama watoto wadogo. Ni dhahiri kwamba nyakati fulani tamaa yao ile ilijitokeza sana, na jambo hilo lilimfanya Paulo kutoa ushauri wake kwamba kila sehemu ya ibada iwe ya kujenga na ifanyike kwa utaratibu mzuri. 1 Wakorintho 14:40. ‘*Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko,*’ aliwaonya, ‘*bali wa AMANI;... KAMA ILIVYO KATIKA MAKANISA YOTE YA WATAKATIFU.*’ Fungu la 33.

Pia si jambo lisilowezekana ya kwamba washiriki wale wa kanisa walitamani kuonyesha kwamba kule kuonekana kwa lugha zeny misisimko katika ibada zile za kipagani kungeweza kuigwa pia katika ibada ya Kikristo. Maneno yasiyo na maana yo yote, wala mshikamano yalitumiwa na watu wote waliokuwa wapagani katika ibada zao.

Sababu na iweje, Wakristo wale wa Kikorintho walionya ili wajizue katika kuonyesha misisimko yao ile kwa habari ya kunena kwa lugha. Ni dhahiri kwamba wengi mno walijitahidi sana - kuipata karama hiyo kuliko zile nyingine. Jambo hilo lilimfanya Paulo kusema hivi: “Basi, *hizi lugha ni ISHARA, si kwao waaminio, bali KWAO WASIOAMINI;* lakini *kuhutubu* [kuhubiri/kutoa hotuba] si kwa ajili yao wasioamini, bali kwa ajili yao waaminio.. Haya! Ikiwa kanisa lote limekusanyika pamoja, na *wote wanene kwa lugha,* kisha ikawa wameingia watu wajinga au wasioamini, *je! hawatasema ya kwamba MNA WAZIMU?*” 1 Wakorintho 14:22,23.

Hapo lugha zinasemekana kwamba ni *ishara* inayothibitisha kwa wale wasioamini kuwa mijumbe yule ni wa kweli, ambapo kuhutubu ni *ishara* kwa *waaminio*. Na wanenaji kwa lugha wanaponena wengi mno kwa wakati mmoja, mwonekano wake ulikuwa kama watu waliorukwa na akili au walio katika mhemuko wa ulevi [kichaa cha ulevi]. Aina hiyo ya maonyesho yaliyojaa machafuko mionganii mwa Wakristo (angalia 1 Wakorintho 14:23,26-33,40) bila shaka lilikuwa ni jambo la kusikitisha sana. Si ajabu kwamba Mtume yule alilazimika kusema, “Basi, ndugu zangu, kwa habari ya karama za roho, sitaki mkose kufahamu. Mwajua ya kuwa mlipokuwa watu wa Mataifa [wapagani], mlitchukuliwa kufuata sanamu zisizonena, kama mlivyoongozwa.” 1 Wakorintho 12:1,2.

Hapo zamani walikuwa wamechukuliwa kwa kufuata taratibu zinazopita kiasi za ibada ya kipagani. Sasa walikuwa katika hatari ya kuwa motomoto kupita kiasi ndani ya kanisa la Kikristo, na jambo lile lingewaongoza katika madanganyo ya Shetani. Karama ya lugha haipaswi kugeuka na kuwa machafuko ya lugha.

Maoni Kadhaa

Sasa tuko tayari kutoa maoni fulani kuhusu karama hiyo ya lugha ambayo Wakorintho wale walikuwa nayo.

- Miongoni mwa karama za kiroho pale Korintho yalikuwapo maonyesho makubwa ya karama ile ya lugha. 1 Wakorintho 14:13,26. Mtume Paulo alidai kwamba aliquwa na karama hiyo. 1 Wakorintho 14:18. Mambo hayo yanaonyesha kuwapo kwa karama ya kweli ya lugha, ambayo haiwezi kupuuzwa kwa kuitumia kupita kiasi na kuitumia vibaya kwa upande wa baadhi ya washiriki wa kanisa.
- Palikuwapo na motomoto uliozidi kiasi katika kutaka kuipata na kuionyesha karama ile ya lugha. 1 Wakorintho 14:23. Jambo hilo lilimfanya Paulo kuwashauri waumini wale ku“tak[a] sana karama zilizo kuu,” kuu kuliko zote ikiwa ni *upendo* wa Kikristo. 1 Wakorintho 12:31; 13:13.
- Karama ya lugha ilikuwa duni kuliko karama ile ya kuhutubu [kuhubiri]. 1 Wakorintho 14:1. Baadhi ya makanisa yale ya mwanzo yanaonekana kana kwamba yalikuwa yamedharau kuhutubu. 1 Wathesalonike 5:20. Korintho huenda ilikuwa na hatia ya kuendeleza karama ile ya kuionyesha ya lugha na kupuuzia karama ile ya kueleza au kutoa ushuhuda wa zile kweli za Injili.
- Kunena kwa lugha kulikuwa ni kusema “na Mungu” mambo ya siri [yasiyoeleweka kwa mnenaji na wasikilizaji], isipokuwa wakati ule pale Pentekoste kunena huko kulipokuwa katika lugha ya nchi nyingine. 1 Wakorintho 14:2. “Siri” katika Warumi 11:25 zilikuwa ni zile kweli za injili zilizokua hazijulikani kwa wale waliokuwa hawajajiunga na kanisa, kweli kama zile za Kukataliwa kwa Israeli na “Utimilifu wa Mataifa.” Katika Warumi 16:25 Paulo anatumia “ufunuo wa ile siri” kwa kuieleza kikamilifu injili kwa njia ya kuhutubu [kuhubiri]. Kama maonyesho hayo ya lugha katika 1 Wakorintho 14:2 yanahusu hotuba au lugha ya Roho inayojulikana tu na Mungu, au kwa njia ya mfasiri aliyechaguliwa naye, basi maoni mawili yanahitimishwa: (a) Jambo hilo lilikuwa tofauti na kumwagwa kwa Roho pale Pentekoste miaka kama ishirini na tano hivi kabla yake; (b) Maonyesho hayo yalikusudiwa kuiimarisha imani ya waongofu wapya, wala sio kumridhisha au kumheshimu mpokeaji wa kipawa kile. 1 Wakorintho 14:22,4. Sababu hizi bado zinatuacha sisi kuwa na fursa ya kulijibu swali hili: Je, karama kama hiyo iliendelea kuwamo katika kanisa la Kikristo katika siku zile za Agano Jipywa na baadaye? Kwa jambo hilo itatupasa kuomba msaada wa kurasa za historia ya kanisa.
- Katika ibada ya kanisa palitakiwa pasiwepo na machafuko yo yote kwa njia ya watu wengi kunena kwa lugha kwa wakati ule ule mmoja, ila alitakiwa anene mmoja kwa muda fulani, kisha anene tu iwapo alikuwapo mtu mmoja wa kuutatafsiria mkutano uliokuwapo pale. *Bila kuwapo mtafsiri [mkalimani], kuwa kimya ilikuwa ndiyo kanuni.* Fungu la 28. Wakorintho wale walikuwa wameivunja kanuni hiyo. Mazoe ya siku hizi [ya kunena kwa lugha] kwa sehemu kubwa hapo ndipo yanapovunja sheria hiyo pia.
- Mazingira yaliyowafanya wengi kunena kwa wakati ule ule mmoja, yanaonekana dhahiri katika hali fulani ya msisimko wa kunena kwa lugha, pamoja au bila ya kuwa na mtafsiri; au hata kwa njia ya karama ya unabii; mambo hayo yanakemewa kwa ukali kwa njia hii: “Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani,... kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu.” Angalia 1 Wakorintho 14:26-33.
- Wakati anawashauri waumini wale wa Korintho ili wapate ku“tak[a] sana karama zilizo kuu” za Roho, Paulo anautukuza *upendo* kama ndiyo “njia iliyo bora” na kukuinua kuhutubu (“yaani, kipawa cha kufafanua mapenzi na makusudi ya Mungu” [1 Wakorintho 12:10, Amplified New Testament]) juu kuliko kunena kwa lugha. Mtume anajaribu kusahihisha matumizi mabaya ya lugha, lakini, hata hivyo, yeze halaumu karama halisi ya lugha kwa kuwa mara nyingine inaweza kujitokeza ile ya bandia

8. Sura tatu zinazofikiriwa hapo (1 Wakorintho 12, 13, na 14) ndizo kumbukumbu za pekee za Maandiko ambazo zinataja karama hiyo ya lugha nje ya zile tulizoziona katika kitabu kile cha Matendo. Jambo hilo linadokeza kwamba karibu na mwaka ule wa 57 B.K. zilipoandikwa hizo Nyaraka za Wakorintho, mpaka kufika karibu na mwaka ule wa 96 B.K., kinavyosadikiwa kuwa ndio mwaka kilipoandikwa kitabu kile cha Ufunuo, karama hiyo ya lugha umuhimu wake ulikuwa ukizidi kupungua sana. Baadaye tutatoa sababu nzuri kwa pointi hiyo.

SURA YA 5

Agano Jipyä Hadi Matengenezo ya Kanisa

Miaka ya Kwanza Mia Nne ya Kipindi cha Kikristo

Sio tu kwamba kurasa za mwisho za Agano Jipyä zimenyamaza kimya kuhusu karama hiyo ya lugha, hata hakuna ushahidi thabiti wa kuwapo kwa karama ile ya kweli katika kipindi cha miaka 200 ya Mwanzo wa Kipindi cha Kikristo.

Kumbukumbu ya kwanza tunayoweza kuipata ni katika kipindi cha Ireneo (Irenaeus), askofu wa Lyoo (Lyons), aliyeuawa kama mfa dini katika mwaka wa 202. Kumbukumbu hiyo inaeleza tu kwamba askofu huyo mwema alikuwa amepata kusikia kwamba mahali fulani walikuwako watu walioongea kwa lugha za kila namna. Mapema kidogo kuliko kipindi kile cha Ireneo, Yustino Mfia-dini (Justin Martyr), ambaye aliihi kipindi kile kimoja pamoja naye, (aliyeuawa mwaka 168 B.K.), alitoa taarifa ya kupata kusikia matumizi ya karama za unabii, lakini yeze hakuzitaja “lugha.”

Waandishi wengine wanawataja Wamontana (Montanists) kwamba walikuwa washabiki wa “kunena kwa lugha.” Walikuwa wafuasi wa Montano (Montanus), mtu wa kikundi fulani cha dini kutoka Frigia wa karne ile ya pili aliyejaribu kurejesha Ukristo wa kawaida na usafi wa maisha, lakini hasa akiwa hana zaidi ya kuwa na juhudzi za kuishi maisha ya kujinyima anasa za mwili ili kukuza karama za roho, sifa hizo anaweza kupewa yeze.

Tertuliano (Tertullian – B.K. 150-230), aliyeshirikiana na Wamontana, alikuwa ni askofu wa Kathage (Carthage). Mionganoni mwa kazi zake [vitabu vyake] nyingi mijadala ni ile inayojulikana sana iitwayo *Against Marcion* [Dhidi ya Marsioni], katika Gombo la 5 na la 8 ambamo anaeleza kwamba huenda “kunena kwa lugha” kulionekana mionganoni mwa wale Wamarsioni.

Mmojawapo wa Mababa wa Kwanza wa Kanisa aliyekuwa maarufu kuliko wote alikuwa ni yule Origeni (Origen – B.K. 185-253), mcha Mungu aliyejulikana kwa maandiko yake ya kufafanua Maandiko. Kitabu chake cha *Hexapla*, kilichopanga kwa safu Maandiko ya Kiebrania na tafsiri zake tano za Kigiriki, yalikuwa ni chanzo cha thamani kwa uchunguzi wa mafungu ya Maandiko. Katika karne ile ya tatu alidai kwamba walikuwapo manabii fulani walionena kwa lugha, lakini maelezo ya kinagaubaga aliyotoa yanadokeza zaidi kwamba walikuwa wakisema maneno ya unabii kuliko kunena kwa lugha, wala haijawa wazi kama alikuwa akiongea juu ya Wakristo au juu ya watu wenye dini mbalimbali nyinezo.

Karibu na mwisho kabisa wa karne ile ya nne mnenaji yule mwenye sauti nzuri, Yohana Krisostomu (John Crysostom – B.K. 347-407), Mzee wa Konstantinopo, aliandika maoni yake juu ya 1 Wakorintho 12 kwa njia ambayo yeze, akiwa anazitaja karama zile za Roho na hasa karama ile ya lugha, alisema:

“Mahali hapa pote hapaeleweki kabisa: lakini kutokuelewka kwake kumesababishwa na ujinga wetu wa kutojua mambo ya kweli yaliyotajwa hapo, na kutokana na kukoma kwake, kama vile yaliwyokuwa yakitokea kwa kawaida wakati ule, lakini sasa hayatokei tena.” Homily XXIX, *The Nicene and Post-Nicene Fathers* (Mababa wa Nikea na Wale Waliokuja Baadaye), Mfululizo wa kwanza, Gombo la 12, uk. 168. Ni kweli kwamba taarifa za kuwako kwa “lugha” hizo mionganoni

mwa makundi fulani zinatolewa, kwa mfano, na Agostino (Augustine) katika karne ile ya nne, lakini ni chache mno, wala hazieleweki wazi kiasi kwamba hazina maana yo yote kuhusiana na hoja yetu hapa.

Ushahidi Huo Unamaanisha Nini?

Huo ndio ushahidi karibu wote unaohusiana na lugha tuweza kuupata, katika baadhi ya karne nne na nusu, na pana umuhimu wa kutaka maelezo fulani yatolewe.

Kwanza, kipindi kile cha kuanzia wakati ule wa Pentekoste mpaka mwisho wa karne ile ya kwanza - yaani, kipindi kile cha Mitume - kilishuhudia kuenezwa mahali pengi kwa Injili kuliko kipindi kinginecho chote kilivyopata kuona. Kilanza kwa ushuhuda wenyewe nguvu kwa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu kwa njia ya karama mbalimbali kwa watu mbalimbali. Ili makundi yote yaliyokusanyika pale Yerusalem yapate kusikia, karama ya lugha ilijitokeza pale. Hiyo ilitimiza kusudi la Mungu katika tukio lile ambalo vile vile lilikuwa ni la pekee. Mbali na kuonekana kwake mara mbili au tatu kwa kiwango kidogo, karama hiyo kuonekana kwake kulizidi kupungua zaidi na zaidi; kisha, baada ya tukio lile lililoendelea kwa mfululizo pale Korintho ambalo tayari tumelichunguza, karibu ilitoweka kabisa katika kumbukumbu za historia zilizoweza kuandikwa. Pengine karama hiyo ya lugha ilikuwa pamoja na Wakristo wale waumini katika kipindi cha robo karne hivi kati ya Siku ile ya Pentekoste na yale matukio ya mfululizo yaliyotokea kule Korintho, lakini hakuna kumbukumbu yo yote ya Agano Jipyä inayothibitisha [kuendelea kuwako kwa] jambo hilo. Kama lugha za mtindo ule wa Pentekoste zingekuwa ni jambo kuu katika kazi ya Roho Mtakatifu, basi, kumbukumbu fulani, zinazotokana na kanuni ya kanisa au zisizokuwa za kanisa, zingekuwa zimetufikia sisi. Lakini, basi, ni kimya.

Je, hilo humaanisha kwamba Roho Mtakatifu alikuwa ameondolewa ndani ya kanisa? Haliwezi kuwa na maana hiyo, kwa maana hicho kilikuwa ndicho kipindi hasa ambacho miujiza ilitokea na mahubiri yenyeye kuzaa matunda yameandikwa katika kitabu cha Matendo, sura ya 3 mpaka ya 12. Kutajwa kuwako kwa Roho Mtakatifu na uweza wake kumeandikwa katika kila ukurasa wa sura hizo. Huo uliokuwa ndio mwanzo wa kipindi maalum katika historia ambacho katika hicho “Neno la Bwana likazidi na kuenea.” Matendo 12:24. Waumini “*wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu [sio lugha] kwa ujasiri.*” Matendo 4:31. Neno la Mungu, likiwa ni injili ya neema iokoayo, lilikuwa likienea kama moto katika kipindi kile. Pia nyaraka nyingi za Kikristo pamoja na kumbukumbu muhimu zilikuwa zikiandikwa; maelfu ya hizo yalikuwa yakienea kila mahali, baadhi yake baadaye zikawa sehemu ya Maandiko Matakatifu. Hakika hiyo ilikuwa ni siku ya [kipindi cha] Roho Mtakatifu ndani ya kanisa, licha ya ukweli kwamba ni dhahiri kwamba ile karama ya lugha ilizidi kupungua kabisa wakati injili ilipoenezwa katika mahali pale palipokuwa mbali.

Pili, kuanzia karibu na mwaka wa 31-63 B.K. kipindi hicho kilichofunikwa na kitabu hiki cha Matendo, ambacho Luka, huenda akiwa Mmataifa, alikuwa ndiye mwandishi wake. Kwa kawaida watu wengi wanakubali kwamba kitabu hicho kinachojulikana kama *Matendo ya Mitume* kwa kweli *ni kitabu cha matendo ya Roho Mtakatifu* kuititia kwa Mitume na waumini wale wa mwanzo. Safari tatu za kimishonari za Paulo - ya kwanza (Matendo 12:24 hadi 14:28), ya pili (Matendo 15:36 hadi 18:22), na ya tatu (Matendo 18:23 hadi 21:17) - zote zinaangukia katika kipindi hicho. Katika kipindi kile cha miaka 100 ya kwanza ya kile Kipindi cha Kikristo waumini wale wa kanisa la mwanzo waliokuwa wakiteswa “wakaenda huko na huko wakilihubiri neno.” Matendo 8:4. Je, tukiacha kisa kile cha kutatanisha cha Wakorintho, twaweza kuthubutu kusema kwamba kwa sababu karama ya lugha inaonekana kidogo zaidi na zaidi katika picha hiyo, basi, Roho Mtakatifu

alikuwa anaondolewa katika kanisa? Ushahidi ni kwamba karama ile ya kweli ya lugha, haikuwa ya kudumu, wala ya kila mtu mahali pote katika Kanisa lile la Kikristo la karne ile ya kwanza.

Tunasonga mbele sasa kwenda kwenye nyakati zile zilizofuata baada ya kanisa lile la Agano Jipy, na baada ya Mababa wale wa karne ya nne.

Historia ya Lugha katika Vizazi vya Baadaye

Ingekuwa ni ufidhuli kudokeza kwamba baada ya vipindi vile tulivyozungumzia habari zake, Mungu hakuitumia tena karama hiyo ya lugha. Naam, yawezekana kwamba alizitumia karama zote tangu siku zile za Agano Jipy kama ilivyompendeza yeze; lakini sisi hatujui habari yo yote juu yake.

Kitabu kile cha mwisho cha Biblia - Ufunuo - labda kilikamilishwa kuandikwa karibu na mwaka wa 96 B.K. Kuanzia pale na kuendelea kwa karne kadhaa maandiko hayo ya Agano Jipy na nyaraka za Kikristo nyingi nyinginezo zilizothaminiwa sana pamoja na maandiko ya mkono yalitawanywa na watu binafsi. Katika karne ile ya nne vitabu vinavyotambuliwa na kanisa vya Maandiko ya Agano Jipy vilikubaliwa na wengi miongoni mwa viongozi wale wa Kikristo.

Msomaji atakuwa amechunguza kwamba wakati ule Biblia ilipoanza kupatikana, karama ile ya lugha ilikuwa inazidi kupungua kutumika miongoni mwa yale makanisa. Na wakati ulipofika wa kuvitambua vitabu vya Biblia vinavyofaa kutumika, karama hiyo ilikuwa karibu imekoma kabisa. Je, yawezekana kwamba Mungu aliona kwamba zile lugha za Pentekoste zilikuwa zikihitajika kidogo mno na kanisa lake, kwa vile sisi tunatakiwa kuishi kwa kanuni zilizo katika hilo Neno Takatifu, tukipata humo maarifa yetu ya kumjua Mungu na ile kweli, pamoja na ule uweza unaotutia nuru na kutuokoa?

“Kuna ... uwezo utendo miujiza katika damu,” tulizoea kuimba wimbo huo. Ni wapi peke yake tunapojifunza habari za damu ile ya “Mwana-Kondoo” iliyomwagwa? Ni katika Neno la Mungu la thamani peke yake. Endapo sisi tungemtumikia yeze kwa kicho, basi, tusingehitaji misisimko mingi sana kwa njia ya karama za nje, kwa kuwa tunao moto wa Mungu ndani ya roho zetu. Ni kweli, Mungu angeweza kuitumia karama yo yote kupitia kwa watumishi wake kama angeona kwamba haja ipo ya kufanya hivyo. Kwamba tunamhitaji Roho Mtakatifu, tunasema tena, ni jambo lisilo na maswali. Lakini swalii lipo endapo tunazihitaji “lugha” kama wanavyodekeza baadhi ya watu kwamba huo ndio ushahidi mkuu unaoonyesha kuwako kwake Mungu [katika maisha yetu].

Zama za Kati

Giza lililochukua kipindi kirefu sana cha takriban [karibu] miaka elfu moja kinatukabili hapa. Wanahistoria wa kidunia kwa kawaida wanakuwa na mashaka kuhusu mambo yasiyokuwa ya kawaida yahusuyo miujiza ya kiroho, nao huyapa nafasi ndogo tu. Wanahistoria wa kanisa pia wamekuwa hawapendi mabadiliko, ama wanakwepa kuyataja mambo kama hayo, ama kuyaeleza kwa moyo wa mashaka. Watetezi wa dini mara nyingi sana wametoa picha iliyotiwa chumvi nyingi sana ya mambo ya kishirikiana na hadithi za kuwazia tu. Kama George W. Dollar anavyooleza katika *Bibliotheca Sacra*, Oktoba, 1963: “Hapa tunashughulika na mambo mengi ya kishirikina yaliyojaa mafumbo, yasiyoelezeka, ya kuogofya, ya miujiza, na ya kitawa ambayo inabidi mtu awe mwangalifu kabisa wakati wa kuyachunguza ili kupata mifano yenye mizizi mirefu katika mambo ya kiroho ya Agano Jipy, na jambo hilo lingekuwa ni la kweli hasa kuhusiana na karama.”

Katika historia ya kanisa wanatajwa watawa fulani walioishi maisha ya upweke katika karne ile ya kumi na tatu na kumi na nne ambao walizungumza lugha nyingine zaidi ya ile waliyozaliwa nayo, na yule Fransisi Kisavia (Francis Xavier), aliyekuwa akijulikana sana katika karne ile ya kumi na sita, alidai kwamba anaweza kuitumia lugha inayojulikana kule India. Lakini hadhari inatakiwa katika kuyakubali madai hayo yasiokuwa na maelezo ya kutosha.

B. B. Warfield, katika kitabu chake cha *Miracles Yesterday and Today* [Miujiza Jana na Leo], ukurasa 127, anaonyesha kwamba Kanisa la Roma linadai kwamba lina “uwezo wa kufanya miujiza kama karama ya kudumu.”

Katika Nyakati za Matengenezo ya Kanisa

Kama kuna kipindi katika historia ya kanisa, tangu ziku zile za Mitume, ambacho tungeweza kutazamia kuona ishara fulani ambayo ingeonyesha ushahidi wa kuwako kwake Mungu, hakika kingekuwa ni kipindi kile cha Matengenezo ya Kanisa ya karne ile ya kumi na sita. Giza la kiroho lilikuwa limeijaza miyo ya watu, licha ya hali ile iliyokuwapo ya ufisadi, mateso, ujinga, na ushirikina. Kanisa lile kuu [Roma] lilikuwa limepoa sana kiroho, tena lilikuwa halina uwezo wo wote. Watu waliokuwa na bidii hapa na pale waliweza kuomba tu, wakisema, “Hata lini, Ee Bwana?”

Ndipo saa ya Matengenezo ya Kanisa ikagonga, na watu waliokuwa wacha Mungu wakahuishwa tena kwa kumwagwa tena Roho Mtakatifu, bila shaka kukiwa ni kumwagwa kukubwa kuliko kote tangu siku zile za Agano Jipy. Siku ile ambayo Lutheri, Melanktoni, Yohana wa Saksoni, mwenye haki ya kumteua mfalme, na wengineo walipotoa itikadi zao za Matengenezo ya Kanisa mbele ya Mfalme yule wa dola, Chalesi wa Tano, imeitwa “siku kuu kuliko zote ya Matengenezo ya Kanisa, na mojawapo mionganoni mwa zile zilizo tukufu sana katika historia ya Ukristo na ya wanadamu.”

Mwamko ule wa karne ile ya kumi na sita ulijulikana sana kwa nguvu ya mafundisho yake ya dini yenye itikadi kama hizi - dhambi, kuhesabiwa haki kwa imani, uvuvio wa Maandiko, ukuhani wa Kristo, na kadhalika. Msisimko wa nyakati zile za kusisimua uliletta mashtaka ya kuvuka mipaka ya imani dhidi ya Waprotestanti, na kwa kweli palikuwa na mifano hapa na pale ya watu walioongozwa kwa misisimko na kurukwa na akili kwa furaha inayobubujika. Idadi fulani mionganoni mwa Waanabaptisti (Anabaptists), wafuasi wa Minsta (Munsterites), na Waalbigensia (Albigenses) wa Languedoc, walisemekana ya kwamba walikuwa ni washupavu wa dimi wasiotumia akili. Lakini, tukiruhusu kuwapo kwa uwezekano wa misisimko inayozidi kiasi katika nyakati fulani za kusisimua, mashtaka mengi sana mionganoni mwa hayo yalilengwa na maadui zao wakali dhidi yao.

Mafundisho ya dini kutoka katika Biblia, yaliyokuwa yamefanyiwa utafiti na kutangazwa kwa uweza wa Roho Mtakatifu, ndiyo yakawa msingi wa yale Matengenezo ya Kanisa. Lakini tunafanya kazi bure kutafuta karama ile ya kweli ya lugha katika mageuzi yale makubwa ya kiroho. Mionganoni mwa wahubiri wote mashuhuri, wataalam wa Biblia, na waandishi waliotokana na Matengenezo yale ya Kanisa, hakuna hata mmoja anayeaminii kwamba karama hiyo ya lugha ilikuwa na sehemu yo yote katika kipindi kile cha uamsho wa kihistoria.

Mara moja tena tunaona ushahidi wa kihistoria unaoonyesha kwamba Roho Mtakatifu alikuwa akitenda kazi yake kwa uweza mkuu *bila kuitumia karama hiyo* [ya lugha] ambayo tunaendelea kuchunguza. Yatupasa kuhitimisha kwamba kule kuonekana kwa karama ya lugha sio ishara peke yake - wala si ya maana kuliko zote - inayoonyesha kuwako kwake Mungu na uweza wake [katika maisha ya Mkristo].

SURA YA 6

Kipindi Baada ya Matengenezo ya Kanisa

Katika Nchi ya Ufaransa na Uingereza

Suala hilo linatufikisha katika nyakazi za siku hizi, ambazo katika hizo, ukilinganisha na miaka elfu moja na mia tano au zaidi iliyopita, [sasa] kuna ushahidi tele wa kuwapo kwa makundi yanayonena kwa “lugha.” Ukiwaacha wale “manabii wadogo” wa Devenne, Ufaransa, mwishoni mwa karne ile ya kumi na nane, wakati watoto wadogo wa miaka mitatu hadi kumi waliposimama na kuhubiri kwa lugha safi ya kifaransa, mfano huu unaofuata wa “kunena kwa lugha” ambao unajulikana sana ulitokea kule Uingereza.

Mchungaji mmoja wa Kipresibiteri kwa jina Edward Irving [Aiving’i], ambaye alizaliwa mwaka wa 1792, alikuwa ni mhubiri mwenye nguvu ambaye alipendwa na watu wengi katika mji wa Landani. Alikuwa na uwezo wa kuhubiri kwa saa nyingi, na mara kwa mara aliomba mbele ya watu kwa dakika thelathini kwa safari moja. Alihubiri juu ya fundisho la marejeo ya Kristo yaliyokuwa karibu sana kwa makundi makubwa ya watu kwa uwezo ulioleta matokeo. Lakini

alikuwa ni mtu mwenye tabia ya misisimko sana, naye aliweka akiba kubwa sana ya uzoefu wake kihisia kama ushahidi wa mbaraka wa Mungu. Yeye pamoja na wale wengine waliomba kwa vipindi virefu ili wapate nguvu mpya ya Pentekoste, na, kwa kweli, mambo yalitokea.

Mmoja mmoja, washiriki wa usharika wake wakasikia kelele za ajabu na maneno yasiyo na maana. Wengine walipatwa na hali ya kupagawa na kuzimia kama wenye kifafa. Wengine walitabiri mambo ya mbele kwa kutumia lugha yao. Wengine waliomba bila kukoma kwa siku nyingi ili wapate “ubatizo wa kunena kwa lugha” au “Pentekoste ya pili.” (Kanisa lile la Presibiteri lilikuwa limekata uhusiano wake na Irving, naye alikuwa anajitegemea.)

Kilichofuata ulikuwa ni ushupavu wa dini wa kuogofya mno ambao ulijimaliza wenyewe. Matukio ya kishenzi [kipagani] chini ya kifuniko cha “kunena kwa lugha” yalijitokeza, na muda mfupi baadaye mitume na manabii wakajitokeza katika kundi lile, wakidai kwamba walikuwa wamerithi utume wao kutoka kwa wale Kumi na Wawili. Mwanamke mmoja kijana, Mary Campbell, alidai kwamba anayo karama ya unabii. “Mafunuo” ya ajabu kabisa yakafuata, kama yale yaliyosema kwamba Vyama vya Biblia vilikuwa ni laana tupu. Hatimaye watu waliokuwa na akili timamu wakajiondoa. Irving aliyejikuwa na kipawa zamani aliona mvuto wake ukipungua sana na kutoweka, na baada ya miaka michache kupita alikufa akiwa mtu mwenye huzuni nyingi. Kile kilichobaki katika vyote kutukumbusha juu ya kundi lile hivi leo ni kanisa dogo mjini Landani, liitwalo *The Catholic Apostolic*, lililo na wafuasi wachache mno na mali kidogo ya kumiliki kule Surrey. Washiriki waliopo leo hawadai kwamba wanao uhusiano wa kindugu na Irving katika kuvuka kwake mipaka, wala hawajali wakikumbushwa juu ya habari hiyo.

Mtu mmoja aliyejiondoa katika mafundisho ya Irving aliandika kitabu chake cha *Narrative of Facts* [Simulizi ya Ukweli wa Mambo], ambamo anasema maneno yafuatayo: “Ilikuwa dhahiri kwangu ya kwamba uwezo ule ulikuwa si wa kibinadamu; kwa hiyo yule alikuwa ni pepo. Kwangu alioneckana kutoa ushuhuda ulioonyesha kazi na matunda ya Roho wa Mungu. Hitimisho likawa haliepukiki, ya kwamba yule alikuwa Roho wa Mungu; na, kama ndivyo, basi, mara moja niliweza kuhisi kuwa ni lazima utii utolewe kwake katika mambo yote.... Kwa hiyo, ni kosa la kufisha kama roho yule adanganyaye [Shetani] anakaribishwa kama Roho Mtakatifu wa Yehova. Kadiri Mkristo aliyedanganywa anavyotumia muda wake mwingi kwa shughuli hiyo, ndivyo kadiri anavyoendelea kutoa utii wake bila maswali kwa roho [pepo] huyo adanganyaye.” - Anderson, *The Gift of Tongues* [Karama ya Lughu], maneno hayo yamenukuliwa toka katika kitabu cha Stolee, *Speaking in Tongues* [Kunena kwa Lughu], ukurasa wa 62.

Watu wanapotangatanga na kwenda mbali na mafundisho ya Neno la Mungu, huku wakiwa wanatafuta uwezo, wanaweza kuingia katika uwanja wa Wamizimu. Wanaweza kuijingiza katika nyanja ambazo kwa hakika watakuwa wanachochea nguvu za kiroho, lakini huyo [anayewaongoza] hatakuwa ni Roho Mtakatifu wa Mungu. Madanganyo kama hayo hayaikanushi kazi ya kweli ya Roho Mtakatifu, lakini yanatoa onyo la kuwapo uwezekano wa kuingia katika madanganyo ya Shetani.

Amerika ya Kaskazini

Kazi ya Uamsho ule Mkuu iliyofanyika chini ya Jonathan Edwards katika mwaka ule wa 1734, ambayo iliungwa mkono na Whitefield, pamoja na anika Tennants, na wengineo, ilipita kama mkondo wa maji kutoka Massachusetts na kuititia katika makoloni yote. Chini ya mahubiri yenye nguvu na yenye kusisimua ya Edwards, ilioneckana wazi misisimko ya kimwili au maajabu katika misuli ya mwili, kama yale yaliyotokea katika karne ile ya kumi na nane katika kazi iliyofanywa na akina Weslii (Wesley). Hisia za moyoni zinazozidi kiasi huleta matokeo kama hayo

nyakati fulani, na yule Jonathan Edwards mara kwa mara alikua na watu waliokuwa wakimsikiliza ambao walikuwa wanapiga makelele na kulia na kuanguka chini kama watu waliokufa. Lakini, hakuna ushahidi wo wote unaoonyesha kwamba watu wale walinenwa kwa lugha, ziwe za kweli au za bandia.

Tapo [Kundi] hilo la Kipentekoste katika nchi ya Amerika lina madhehebu kama arobaini na tano hivi [kufikia mwaka wa 1965] ambazo huipa kipaumbele karama hiyo ya kunena kwa lugha kama sehemu ya ibada. Wako katika kila jumbo linalojitawala na katika nchi za ng'ambo, nao wamekua na kuongezeka kwa haraka sana. Dini kama hiyo ni ngeni kwa ulinganifu katika maisha ya kidini ya Kiamerika. Ni dhahiri kwamba dini hiyo haikuwako mionganoni mwa Mababa wale Wasafiri (Pilgrim Fathers), Wapyuritani (Puritans), Wapresibiteri (Presbyterians), Wamethodisti (Methodists), au wengineo wa nyakati zile za mwanzo. Kiasi kidogo cha dini hiyo kilionekana mionganoni mwa wafuasi wa Weslii, lakini hawakudumu kwa muda mrefu. Wamomoni (Mormons) ni mionganoni mwa watetezi wa kwanza wa "kunena kwa lugha," kwa sababu Joseph Smith alipokea maono na mafunuo, naye aliiamini karama hiyo ya lugha, walau kwa njia ile kilivyomjia kile Kitabu cha Wamomoni (*Book of Mormons*). Mwasisi wa dini ya Masheka (Shakers), "Mama" Ann Lee, alidai kwamba alizijua lugha zaidi ya sabini. Washiriki wote katika mkutano wa ibada waliweza kucheza dansi na kupiga makelele kwa furaha, na katika kipindi cha kufanya mambo hayo ndipo nyimbo zao nyingi za dini zilipotungwa, ingawa ziliwuwa na maneno yasiyo na maana yo yote.

Washiriki wa vikundi vya "kunena kwa lugha" kwa kawaida hawapendi kukumbushwa juu ya matukio yale yanayohusiana na kile kilichodhaniwa kuwa ni karama ya lugha katika Majimbo yale ya Kusini [ya Amerika]. Tunapoyagusia hapa kusudi letu ni kuonyesha tu hatari za kuvuka mipaka zinazotokana na tamaa ambazo kwa upande mwingine zinafa kwa watu wenye ari.

Pale Inezi, Kentucky, mwaka ule wa 1933, kundi moja lenye taratibu za ibada za ajabu-ajabu liliamsha maoni yaliyoenea mahali pengi, kama haya yafuatayo:

"Kundi hilo lilijilingiza katika utaratibu wa ibada ya ajabu sana iliyopewa jina la 'kifo cha dhambi.' Baada ya kipindi fulani cha kufunga [kuacha kula chakula], walianza kucheza dansi, kuimba nyimbo za kunuizia uchawi [ushirikina], na kunena katika lugha zisizojulikana, wakiendelea kufanya hivyo kwa karibu juma moja hivi, ndipo mwanamke mmoja kizee, Bibi Lucinda Mills, alipochaguliwa kuwa kafara ya kibinadamu, naye aliuawa kwa kukatwakatwa vipande vipande na mwanawewe, John H. Mills. Ilisemekana ya kwamba maandalizi yalikuwa yanafanywa ya kuuchoma mwili wake juu ya madhabahu ilijoengwa ovyo ovyo tu wakati maaftisa [wa serikali], wakiwa wamevutwa na makelele yale, walipokivamia kibanda kile zilipokuwa zinaendelea taratibu zao za ibada. Wanawake wengine watatu walikuwa wamechaguliwa ili wapate kukabiliwa na ajali kama ile. Mahakamani yule Mills alitoa sauti tu zinazotoka kooni zinazofanana na lugha ile isiyojulikana, wakati wahudumu wake walipokuwa wakiushikilia mwili wake uliokuwa ukijinyonganyonga juu ya kitanda kidogo." - Elmer T. Clark, *The Small Sects in Amerika* [Vikundi Vidogo vya Dini katika Nchi ya Amerika], toleo lililofanyiwa masahihisho, 1949.

Madhehebu nyingi zilijitokeza mnamo mwaka ule wa 1900, zikiwa na malengo yao haya ya utakatifu, kutokuwa na dhambi kabisa, ukamilifu, uwezo wa kiroho. Mengi sana mionganoni mwa hayo yalimilia Mungu ili apate kuzirudisha zile karama, hasa ile ya kunena kwa lugha. Makundi yalitokea kule Virginia, Tennessee, na Kentucky, yakidai kwamba maneno haya ya Kristo yalikuwa yametimizwa kwao: "Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Marko 16:18. Baadhi ya makundi hayo yaligeuka na kuwa "madhehebu ya kushika nyoka," ambayo yalivuka mpaka kiasi kwamba baadhi ya majimbo yalipiga marufuku kushika-shika nyoka wakati wa ibada za dini. Desturi ya

“kunena kwa lugha” imeendelea bila kuvurugwa, na katika mifano fulani fulani hawajionyeshi sana, taratibu zao za ibada ni za heshima zaidi.

Kundi moja kule Topeka, Kansas, mwaka wa 1900 lilipania kujifunza Maandiko, lakini hawakujifunza sana isipokuwa “ubatizo wa ishara” wa kiroho. Muda si mrefu “kunena kwa lugha” kukatokea na misisimko mingi ikafuata, mpaka mwishowe viongozi wake wakapata sifa mbaya. Baada ya pale mji wa Los Angeles ukawa kituo kikuu cha dini kama hiyo, iliyojulikana sana ni ile ya ‘The Old Azusa Street Mission,’ ambako wafuasi wake walidai kwamba walikuwa wameileta “Pentekoste ya pili.” Baada ya muda kupita misheni ile duni ikatoweka, na mahali pake pakachukuliwa na mahekalu ya kisasa ya kifahari zaidi, ingawa ibada zake bado ziliendelea kuwa zenye kuzidi kiasi, na ishara za kimwili kama vile kuponya wagonjwa na kunena kwa lugha zilitiliwa mkazo.

Si kwa uchache ndani ya matapo [makundi] hayo yanayotafuta karama za Roho Mtakatifu zinazoonekana waziwazi kumetokea mambo yanayosikitisha katika nyanja za kimaadili, kiakili, na maisha ya nyumbani. Si lazima kueleza mengi zaidi ya kutaja tu mifano mingi ya usherati na kichaa ambayo inaweza kupatikana katika kazi [vitabu] zinazoweza kupatikana kwa urahisi juu ya somo hili.

Mambo Yaliyonipata Mimi

Wakati wa Vita Kuu ya Kwanza, kwa muda mwingu nilikuwa katika kikosi [kombanii] cha kundi fulani la watu ambaa mionganii mwao ilikuwamo idadi ya waumini wa imani ya Kipentekoste. Walinisonga sana ili niwe na mawazo yaliyo huru na kuhudhuria kanisani kwao. Safari moja nilikwenda na kujaribu kutathmini uzoefu wangu bila kupendelea upande wo wote kwa kadiri ilivyowezekana.

Palikuwa na kuimba nyimbo kwingi sana, ambazo taratibu ziliongezeka kasi yake, pamoja na kupiga makofi na kukanyaga-kanyaga miguu chini. Halafu likaja ombi lilioingiliwa na matamko mengi yaliyojaa msisimko kutoka kwa mkutano. Kwa zamu likaja somo fupi la vifungu vya Maandiko vinavyohusu Pentekoste na karama za roho. Halafu misisimko yenye kina ikalipuka na kuniacha nimepigwa butwaa wakati mmoja baada ya mwininge alipota ushuhuda wake na kutushauri akisema, “Jitoe kwa Roho!” “Jisalimishe kwa Bwana!” Watu wengi mionganii mwao wakaanza kupiga makelele na kupiga makofi. Halafu wengine wakaanza kusema maneno kwa nguvu ambayo sikuweza kuyaelewa kabisa, na wengine walimunyamunya [walisema bila kutamka maneno vizuri wakiwa wamefumba midomo yao] na kutoa mlio wa huzuni kana kwamba wana maumivu fulani. Mwishowe wengine walianguka sakafuni na kulala pale wakiwa wamekauka kama mti na macho yao yakig’aa kama kioo. Wengine walikuwa na misisimko ya “kushtuka mwili mara kwa mara.” Nilijisikia nimo katika mkabala wa uwezo uliokuwa mgeni sana kwa hisia za dini yangu, nikatoka nje kuingia ktika hewa safi ya Mungu nikiwa siamini hata kidogo kwamba kuwapo kwake Mungu kulikuwa katika mkutano ule.

Laiti kama watu hao wangkuwa wameyaelewa maneno haya ya Paulo katika 1 Wakorintho 14:27,28: “Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena *zamu kwa zamu*, na *mmoja na afasiri*. Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na *anyamaze katika kanisa*; aseme na nafsi yake tena na Mungu.”

Baada ya kupatikana na mambo hayo niliweza kusadiki kile kilichokuwa hakisadikiki kabla ya hapo. Nilikuwa nasoma taarifa za milipuko kama hiyo ya misisimko inayozidi kiasi ambayo inaambatana na kupiga makelele na kuugua [kulia bila kutoa maneno kama mtu anayepata maumivu makali] kulikoonekana kule Kusini, ambako wanawake waliingia katika “mshtuko wa

viungo vyao vya mwili mara kwa mara” ambao ulikuwa na nguvu nyingi sana kiasi kwamba “nywele zao ndefu zilizokuwa hazijafungwa ziliweza kukatika kwa mlio unaofanana na ule wa mjeledi wa kuchapia farasi katika gari linalovutwa na farasi.” Angalia Clark, *The Small Sects in Amerika*, toleo lililofanyiwa masahihisho, 1949, uk. 93. Baada ya kujionea mimi mwenyewe, mashaka yangu yamepungua sana kuhusu kile nilichozoea kufikiri kuwa kilitokana na taarifa zilizotiwa chumvi nyingi sana na maadui zao. Kwa hali ya kusikitisha mno taarifa hizo ni za kweli.

Ishara za uongo na misisimko mingi sana, kusema kweli, haikanushi ukweli ule usemao kwamba Mungu alitoa karama zake kwa kanisa lake. Endapo leo hii badala ya kuwa na misisimko, itokanayo na mawazo yaliyomo moyoni mwetu yanayotokana na wasiwasi wetu na azma zetu, tungekusanyika pamoja kwa unyenyekevu na kimya, kujifunza Neno la Mungu ili kuijua ile kweli ya Mungu na mapenzi yake kama walivyofanya waumini wale katika chumba kile orofani (Matendo 1:14; 2:1), basi, mikutano hii isiyokuwa na utaratibu na isiyojenga ya “kunena kwa lugha” ingetoweka. “Mambo yote na yatendeke kwa kusudi la kujenga” [kuimarisana kiroho]. 1 Wakorintho 14:26.

Kitu kimoja kutokana na yale yaliyonipata huwa hakitiliwi mkazo mara nyingi. Endapo mimi ningendelea kubaki mle ndani na kuendelea kuhudhuria mikutano ile na kujiachia mwenyewe kushawishika kufikiri kwamba mimi “nilikuwa nahitaji kupata uwezo ule wa Roho,” basi, muda si mrefu kitu fulani kingekuwa kimeamshwa ndani yangu. Huenda mimi ningekuwa mhanga [mwathiriwa] wa kile ninachoamini kweli kweli kuwa ni uzoefu udanganyao wa kimwili na kiakili ambao unaleta madhara katika akili ya mtu na utulivu wake wa moyo. Midundo [ridhimu] ile inayorudiwa-rudiwa, mazingira yale yaliyojaa misisimko mingi, na mzigo mzito wa wasiwasi unaotaka kutoka moyoni ambao unatokana na shinikizo la maisha ya siku hizi, azma ya kibinadamu ya kutaka “kupata” kitu fulani kipyaa na cha kimapinduzi [kinachobadilisha maisha kabisa] - hiyo ndiyo milango mikubwa ambayo kuitia katika hiyo madanganyo ya Shetani yanaiteka kirahisi mioyo yetu ya kibinadamu.

Hata wainjilisti wale wanaofuata zaidi desturi zilizopo mara nyingi wanatumia mbinu zile zinazochochaea hisia za moyoni isivyostahili ili kuwa kitu kimoja (en rapport) na mkutano. Ni uangularifu ulioje wahubiri wanatakiwa kuwa nao ili wasifanye mambo kupita kiasi kwa kutumia vielelezo na hila, vikorokoro vinavyoonekana, na kuacha maelezo thabiti yaliyojengwa juu ya Kristo, yaani, yaliyojengwa juu ya Biblia, ya kuzifanua zile kweli za milele kwa watu.

SURA YA 7

Je, Itakuwako Pentekoste Nyingine?

Unabii na Suluhisho la Matatizo Yetu

“Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwako na nyakati za dhiki kubwa na taabu - ngumu kuzikabili na ngumu kuzistahimili.” 2 Timotheo 3:1, Amplified New Testament [Agano Jipy Liliokuzwa].

Paulo katika mafungu matatu yanayofuata anaendelea kuonyesha picha ya kuwapo ubinafsi, tamaa isiyozuilkia ya kupenda fedha, majivuno, ufidhuli, kujisifu, kutukana, kutowaheshimu wazazi, kukosa shukrani, kuishi maisha maovu, lugha chafu, ukatili, kashfa, mashtaka ya uongo, uasherati, chuki kali sana dhidi ya mema, usaliti, tamaa mbaya za mwili, dini ya desturi tu na kukosa uwezo, unafiki - mambo yote hayo yatakuwa ndiyo hali itakayokuwako katika “siku za mwisho.” Kuna mengi zaidi ya hayo, na msomaji angepaswa kusoma kwa makini mistari saba ya kwanza ya sura hiyo.

“Siku za mwisho” ni kifungu cha maneno kilicho na maana sana. Mto maoni ajulikanaye sana, asema hivi: “Idadi kubwa ya wale wanaotoa maoni yao wamezitaja ‘siku za mwisho’ zilizotajwa hapo kuwa ni kipindi kile kinachotangulia muda mfupi tu kabla ya kuja kwa Bwana wetu mara ya pili - siku moja na saa moja mahali fulani katika siku za usoni, lakini iliyojificha, sio tu kwa wanadamu wote, bali kwa malaika, na hata kwa Mwana (Marko 13:32).” - *Ellicott’s Commentary*.

Wakristo wengi wanasadiki kwamba wasiwasi unaozidi kuongezeka pamoja na hali mbaya mno za maisha ya nyakati zetu hizi husonda kidole chake kwenye ule mwisho wa mambo yote. Wanatazamia kuja wa Bwana Yesu Kristo kuwakomboa wenye haki na kuwahukumu waovu mionganoni mwa wanadamu.

Kabla ya wakati ule kufika kutakuwako na *kumwagwa kwingine kwa Raho Mtakatifu*, kama wakati ule wa Pentekoste. Wakati ule wa Pentekoste Wakristo waliposhtakiwa kwamba walikuwa wamelewa, mtume Petro alipaza sauti na kuwaambia hivi wale wenye dhhika, “Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi nyote mkaao Yerusalem, lijueni jambo hili,... Sivyo mnavyodhani; watu hawa hawakulewa,... lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli; *Itakuwa siku za mwisho*, asema Mungu, *nitawamwagia watu wote Raho yangu*, na wana wenu na binti zenu *watatabiri*, na vijana wenu *wataona maono*; na wazee wenu *wataota ndoto*. Naam, na siku zile *nitawamwagia watumishi wangu wanaume na wanawake Raho yangu*, nao *watatabiri*.” Matendo 2:14-18.

Hayo yalikuwa ni matumizi [kutimizwa kwa sehemu] ya kwanza ya unabii ule wa Agano la Kale kwa nyakati mpya. Je, kuna matumizi [kutimizwa kwa sehemu] yake ya pili na utimilizo mkubwa zaidi mbele yetu katika nyakati za siku zetu hizi?

Yaonekana kuwa ni jambo la busara kwamba Mungu wa upendo na rehema asingeweza kuutumbukiza kwa nguvu ulimwengu huu katika hukumu ile ya kuogofya mno bila ya kutoa kila onyo linalowezekana kwa mwanadamu. Na kama Mungu aliwatumia Wakristo wale wa mwanzo

kutoa ishara na maonyo kwa kizazi chao kile, je! hataweza kuwatumia tena Wakristo kutoa ishara zake za onyo na maajabu kwa kizazi kile cha mwisho cha wanadamu?

Tena, ikiwa ulimwengu ule wa Kigiriki-Kirumi ulipewa ishara za pekee kwa njia ya karama za Roho Mtakatifu zilizotolewa kwa kanisa lile changa sana, kwa nini Mungu asizitumie karama zile zile kwa uwezo ulioongezeka katika ulimwengu huu unaoelekea hukumuni? Hakika hali iliyopo leo inataka kuwe na ishara fulani za Mungu zinazozidi zile walizokuwa nazo wakati ule wa Pentekoste ile ya kwanza.

Ishara za Mungu Zitakuwa Zaidi ya Zile za Pentekoste

Makundi mengi ya Kikristo yanatarajia kurudi kwa Kristo kutokea kabla ya miaka ile elfu moja, nao wanashikilia kwamba kanisa na ulimwengu vitahusika katika uamsho wa kiroho utakaotokea kabla halijatokea tukio lile la kimapinduzi.

Yohana aliandika kwamba “roho chafu [mashetani/mapepo]” zingekwenda ulimwenguni, kwa maana, “Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara [miujiza], zitokazo na kuwaendea wafalme [na Ma-Rais] wa ulimwengu wote *kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.*” Ufunuo 16:14.

Tafsiri ya Agano Jipyä Lililokuzwa (Amplified New Testament) inasomeka hivi: “Nazo zinatoka na kuwaendea watawala na viongozi ulimwenguni kote, kuwakusanya pamoja kwa vita katika siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi.”

Hakuna kitu kinginecho chote, isipokuwa *kumwagwa kwa nguvu kwa Roho Mtakatifu*, ambacho kingeweza kuipinga mivuto ya kishetani iliyoelezwa hapo.

Hapo ndipo karama za Roho zitakapotolewa upya kwa watu wa Mungu walijitoa wakf kwake. Ni nani atakayesema kwamba karama ile ya kweli ya lugha, iliyio kinyume na ishara zile za uongo za kunena kwa lugha ambazo tumezitaja nyuma, haitakuwa tena ishara-ya-karama itokayo kwa Mungu kupitia katika kanisa lake ili kuwazuia na kuwaonya wale wasiomcha Mungu juu ya hukumu ile inayokuja?

“Matukio ya Siku ile ya Pentekoste yatarudiwa tena kwa uwezo mkubwa zaidi katika tukio lile. Yohana asema hivi, ‘Nalionna malaika mwingine [mvua ya masika/kumwagwa tena kwa Roho Mtakatifu], akishuka kutoka mbinguni, mwenye mamlaka kuu [uwezo mkuu]; na nchi ikaangazwa kwa utukufu wake.’ [Ufunuo 18:1.] Wakati ule, kama katika majira yale ya Pentekoste, watu watasiaka kweli ikinenwa kwao, *kila mtu katika lugha aliyozaliwa nayo.*” - *The Seventh-day Adventist Bible Commentary*, gombo la 6, uk. 1055.

Kwa kweli, hakuna dokezo lo lote hapo kwamba “kunena kwa lugha” kutakuwa ni kitu cho chote kingine zaidi ya uwezo wa kuzihubiri zile kweli za injili ziokoazo kwa “kila taifa na kabilia na lugha na jamaa.” Ufunuo 14:6.

Muhtasari na Hitimisho

1. Je, karama ya lugha ilikuwa ndiyo karama peke yake?

1 Wakorintho 12:11. Mungu alitoa karama mbalimbali “*akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.*” N.E.B. [Biblia ya Kiingereza Kipyä].

1 Wakorintho 12:29,30; 14:5. Karama ya lugha si ya maana kuliko zile nyininge, kwa sababu imewekwa ya pili kutoka mwisho katika orodha zilizo katika 1 Wakorintho 12:8-10,28-30.

Wala haikumfanya yule aliyeipokea aheshimiwe na Mungu au na mwanadamu kuliko wale wengine. Tena, *hakuna ushahidi wo wote unaoonyesha kwamba mtu aliyejazwa na Roho ni*

lazima awe na karama hiyo ya lugha. Askofu Paiki (Pike), aliyetajwa katika sura ya kwanza ya kitabu hiki, aliteua tume ya uchunguzi, nayo ilitoa maonyo dhidi ya kufundisha kwamba “glossolalia [kunena kwa lugha] ndiyo ishara ya lazima inayoonyesha kuwako kwake Mungu na kwamba wale wasiokuwa nayo kwa maana iwayo yote ile ni raia wa daraja la pili wa ufalme wake.”

2. Je, kwa nini karama ya lugha ilitolewa?

Matendo 2:1-11. Ili watu kutoka katika nchi nyingi wapate kusikia habari njema za wokovu.

1 Wakorintho 14:22. Kuwa ishara kwa wasioamini, hasa kwa Wayahudi wasioamini. Angalia Matendo 2:5. Miaka michache baadaye Paulo na Barnaba waligeuka na kuwaacha Wayahudi na kuipeleka injili kwa Mataifa, kama ilivyoelezwa waziwazi katika Matendo 13:46: “Ilikuwa lazima neno la Mungu linenwe kwenu kwanza; lakini kwa kuwa mnalisukumia mbali, na kujiona nafsi zenu kuwa hamkustahili uzima wa milele, angalieni, twawageukia Mataifa.”

1 Wakorintho 14:26. Kama karama zile zote zilivyo, karama ya lugha, alisema Paulo, ni lazima iwe kwa kusudi la “kulijenga kanisa.” Karama ya lugha pia ilikuwa kwa kusudi la kuleta faraja, faida, baraka, shukrani, ndani ya kanisa. 1 Wakorintho 14:3,6,16,17.

3. Je, palikuwa na tofauti yo yote kati ya karama ya lugha iliyotolewa wakati ule wa Pentekoste na ile ya Korintho?

Matendo 2:7-9. Siku ile ya Pentekoste, wote ambao walikuwa hawawezi kuzungumza lugha (ya Kiaramu) waliyoitumia wale Mitume wakati wa kutoa ushuhuda wao, sasa wakaweza kuwasikia Wagallaya wale (ambao walikuwa na ustaarabu duni) *wakihubiri katika lugha za Wayahudi wale waliokuwa si wakazi wa nchi ile, au wale wa Utawanyiko.* Kinyume chake, kule Korintho *hakuna lugha maalum zinazotajwa*, na sehemu kubwa ya washiriki wale inavyoonekana walikuwa si Wayahudi.

Pale Pentekoste *hakuna wafasiri wo wote waliotajwa au waliohitajika*, ambapo kule Korintho Paulo alisisitiza kwamba kile kilichonenwa na Roho Mtakatifu mioyoni mwa waumini wale *kilipaswa kufasiriwa*. 1 Wakorintho 14:13,27.

Matendo 2:6-11. Pale Pentekoste palikuwa na mshangao kutohana na mahubiri yaliyotolewa kwa lugha ndani ya nyumba ile na inavyoonekana hata katika mitaa, hapakuwa na ushahidi wo wote wa kuwapo machafuko. Katika makanisa ya Korintho palikuwa na *machafuko na kuzidi kiasi*. 1 Wakorintho 14:26-33.

Matendo 2:6. Pale Pentekoste *wasikilizaji walielewa kilichozungumzwa*. Kule Korintho nyakati fulani *wanenaji walitamka maneno yasiyokuwa rahisi kuyaewa*. 1 Wakorintho 14:9.

4. Je, palikuwa na mifano ya kujazwa Roho Mtakatifu bila kuwa na karama ile ya lugha?

Matendo 6:5-8, KJV. Stefano alikuwa ame “jaa imani na Roho Mtakatifu”; “akijaa imani na uwezo.” Alikuwa “akifanya maajabu na ishara [miujiza],” lakini yeye, kulingana na kumbukumbu inavyosema, alikuwa hana karama ya lugha, zaidi ya kuwa na karama ile ya kuitumia vizuri kwa utukufu wa Mungu lugha ile aliyozaliwa nayo.

Matendo 10:38. “Habari za Yesu wa Nazareti, jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu.” Alitenda mema kila mahali, akiwaponya hata wale waliokuwa wamepagawa na pepo, lakini alizungumza lugha ile tu aliyozaliwa nayo ya Kiaramu, kwa kadiri sisi tunavyojua.

Marko 16:15-20. Wanafunzi wake “wakahubiri kote-kote,” na mara nyingi walibishana nao na kuwapinga. Ndipo Mungu akawatumia ili wapate kuwagusa watu kwa uthibitisho wa “ishara zilizofuatana nao.” Hakuna kumbukumbu zo zote zinazotaja kwamba wa “linena kwa lugha.”

5. Je, karama ile ya lugha ilitumika tu wakati ule lugha za mataifa mengine zilipohusika?

Matendo 2:4-23; 10:46; 19:6. Ushahidi unaonekana wazi kwamba pale Pentekoste lugha zile za nchi nyingine zilizokuwa zinajulikana zilitumika, ambazo yule mnenaji alikuwa hana ujuzi nazo kabla ya wakati ule. Katika mfano ule wa Kornelio na wale watu kumi na wawili wa Efeso ushahidi hauko wazi. Huenda palikuwa na karama ya pekee ya sifa na maombi, yaani, kumtukuza Mungu kwa njia fulani mpya.

1 Wakorintho 12-14. Kule Korintho mtume anaonekana kana kwamba wakati fulani anaongelea habari za lugha zinazojulikana, na wakati mwengine juu ya maneno yaliyojulikana na Mungu kama sio mnenaji. Maneno yale yalimjenga mnenaji. Angalia 1 Wakorintho 14:4. Lakini hoja nzima ya sura hizo tatu sio juu ya lugha gani ilizungumzwa, bali kwamba ni lazima pasiwe na machafuko, kuvuka mipaka, au kuitumia vibaya karama ile. Ni hakika kwamba Paulo hakatazi kunena kwa lugha, ingawa anahafifisha umuhimu wa karama hiyo ikilinganishwa na upendo na kuhutubu.

6. Je, hivi karama zote za Agano Jipy a zimo ndani ya kanisa la leo?

Si katika mfumo au kiwango cha kanisa lile la kwanza la Agano Jipy. Karama za Roho kama zilivyoordheshwa katika 1 Wakorintho zilianza kupungua taratibu, na nyingine kutoweka, katika karne ile ya pili kabla ya kukubaliwa kwa kanuni ya vitabu vilivyochanguliwa vya Maandiko. Lakini baadhi ya karama hizo zimekuwa pamoja na watu wa Mungu sikuzote. Hata karama hiyo ya lugha imekuwa pamoja na kanisa katika mfumo mwengine, isingekuwa hivyo, je, kwa jinsi gani kweli zile za injili zingeweza kuifikia karibu kila nchi kwa njia ya wamisionari?

Taarifa za karama ya lugha katika hali fulani ya kimwujiza zimekuwako katika nyakati mbalimbali tofauti; lakini, kama zilivyo taarifa juu ya uponyaji, kwa kawaida ni vigumu kuzihakikisha. Maongozi ya Mungu bila mashaka yo yote yamezidhihirisha karama za uponyaji na za lugha wakati wa hatari, yaani, wakati upeo wa uwezo wa kibinadamu unapokuwa umefikia mwisho wake.

Uwezekano upo wa kujishughulisha sana na *karama* za Roho zinazoonekana kwa nje kuliko kushughulika na yale *matunda ya Roho* yanayokwenda chini zaidi. Angalia Mathayo 7:5-20; Wagalatia 5:22,23.

7. Je, zipo karama za bandia, hasa katika siku hizi za mwisho?

Ufunuo 16:14,15; Mathayo 24:24. Roho za mashetani zinaweza kuigiza kazi ile ya kweli ya Roho na kuwadanganya, yamkini hata walio wateule, kama hawakeshi.

1 Yohana 4:1; Isaya 8:20. *Ni lazima tuzipime roho kwa kutumia kanuni za Neno la Mungu ili kuona kama “zimetokana na Mungu;* kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani.” Hilo ndilo jambo la maana sana kufanya kuliko kutumia kipimo cho chote cha kibinadamu au maonyesho [miujiza] ya aina yo yote, haidhuru yawe ya kusisimua jinsi gani. Ni kwa kanuni ile tu ya Neno la Mungu, likitumiwa kwa halali [2 Tim. 2:15], tunaweza kuzitambua zile *karama za kweli*.

VYANZO VILIVYOTUMIKA

- Clark, Elmer T., *The Small Sects in America.*
Cutten, G.B., *Speaking With Tongues.*
Haskett, W. J., *Shakerism Unmasked.*
Hillis, Don W., *What Can Tongues Do for You?*
Mackie, Alexander, *The Gift of Tongues.*
Mayer, F. E., *The Religious Bodies of America.*
Roberts, Alexander, na James Donaldson, editors, *The Ante-Nicene Fathers*, Vols. 1,5,6.
Robertson, *That Old-Time Religion.*
Schaff, Philip, editor, *The Nicene and Post-Nicene Fathers*, Vol. 12.
Sherrill, John, *They Speak With Other Tongues.*
Stolee, H. J., *Speaking in Tongues.*

Stott, John, *The Baptism and Fullness of the Holy Spirit*.
Warfield, B. B., *Miracles Yesterday and Today*.